



ISSN 0856-6976

TAMKO LA SERA YA FEDHA

2026/27

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

Juni 2026



ISSN 0856-6976

TAMKO LA SERA YA FEDHA

2026/27

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

Juni 2026



9 Juni 2026

**Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb),
Waziri wa Fedha,
Mji wa Serikali-Mtumba,
Barabara ya Hazina,
S.L.P 2802,
40468 Dodoma.**

Mheshimiwa Waziri,

BARUA YA WASILISHO

Kifungu namba 21, kifungu kidogo cha (3) hadi (6) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, kinaitaka Benki Kuu kutoa **Tamko la Sera ya Fedha** mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka ambayo hutolewa mwezi Februari. Tamko hili huainisha mwelekeo wa sera ya fedha na utekelezaji wake katika kufikia malengo ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali. Kwa muktadha huo, nawasilisha kwako **Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2026/27**, kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Tamko hili la Sera ya Fedha linatoa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake kwa mwaka 2025/26. Aidha, Tamko hili linabainisha mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, pamoja na mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2026/27 katika kufikia malengo yake.

Wasalaam,

Emmanuel M. Tutuba
GAVANA
Benki Kuu ya Tanzania



YALIYOMO

BARUA YA WASILISHO	i
MUHTASARI	iv
SEHEMU YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI	1
SEHEMU YA PILI	4
2.0 MSIMAMO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA	4
2.1 Msimamo wa Sera ya Fedha	4
2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha	4
SEHEMU YA TATU	8
3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA	8
3.1 Mwenendo wa Shughuli za Uzalishaji	8
3.2 Mfumuko wa Bei	9
3.3 Mwenendo wa Bei za Bidhaa	13
3.4 Mwenendo wa Masoko ya Fedha Duniani	16
SEHEMU YA NNE	18
4.0 HALI YA UCHUMI NCHINI	18
4.1 Pato la Taifa	18
4.2 Mfumuko wa Bei	21
4.3 Viwango vya Riba	25
4.4 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi	27
4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali	30
4.6 Deni la Taifa	33
4.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje	34



4.8	Ukwasi wa Fedha za Kigeni, Thamani ya Shilingi na Akiba ya Fedha za Kigeni	41
4.9	Mwenendo wa Sekta ya Fedha	44
4.10	Mifumo ya Malipo	45
	SEHEMU YA TANO	49
5.0	MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI	49
5.1	Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia	49
5.2	Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani	50
	SEHEMU YA SITA	52
6.0	SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27	52
	VIAMBATISHO	55
	TAFSIRI YA DHANA MUHIMU	63



MUHTASARI

Malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha

Mwezi Juni mwaka 2025, Benki Kuu ilitoa Tamko la Sera ya Fedha ikibainisha kuwa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26 italenga kuongeza ukwasi ili kuwezesha ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Mwelekeo huo ulitokana na matarajio ya mfumuko wa bei nchini kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Hivyo, katika utekelezaji, mwezi Julai 2025 Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilipunguza Riba ya Benki Kuu kutoka asilimia 6 hadi 5.75 katika robo mwaka inayoishia mwezi Septemba 2025, na kubaki katika kiwango hicho kwa kipindi kilichofuatia cha mwaka 2025/26. Aidha, katika kuongeza ufanisi wa sera ya fedha na kuhakikisha malengo ya sera ya fedha yanafikiwa, Benki Kuu ilipunguza wigo wa CBR kutoka asilimia 2 hadi 1.5 kuanzia mwezi Aprili 2026, sambamba na kufanya maboresho na kutoa mwongozo wa mfumo wa dhamana, ili kuweka mazingira wezeshi kwa benki kupata ukwasi, kupitia mikopo ya muda mfupi inayotolewa na Benki Kuu.

Matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yalikuwa ya kuridhisha, ambapo mfumuko wa bei ulibaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 kama ilivyotarajiwa, huku ukuaji wa uchumi ukiendelea kuwa wa kasi na imara, licha ya athari zilizotokana na migogoro ya kisiasa Mashariki ya Kati. Aidha, matokeo hayo yametokana na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, yakiakisiwa na riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabanki kubaki ndani ya wigo wa Riba ya Benki Kuu.



Mwenendo wa uchumi wa dunia

Uchumi wa dunia katika mwaka 2025, ulikabiliwa na changamoto zilizotokana na migogoro ya kisiasa, kuongezeka kwa ushuru wa forodha kwa baadhi ya nchi, na kutotabirika kwa sera za kiuchumi. Licha ya changamoto hizo, uchumi wa dunia ulikuwa stahimilivu, ukikua kwa asilimia 3.4 mwaka 2025 kwa mujibu ya makadirio ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Februari 2026. Hata hivyo, kuanzia mwezi Machi 2026, mfumuko wa bei ulianza kuongezeka kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi, kutokana na mgogoro wa kisiasa Mashariki ya Kati. Hali hiyo ilisababisha kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta, na hivyo kuongeza mfumuko wa bei. Aidha, kufuatia matarajio ya kuendelea kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, benki kuu nyingi zimesitisha mipango ya kupunguza riba za sera ya fedha.

Mwenendo wa riba katika masoko ya fedha duniani haukuwa wa kutabirika katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026. Hali hiyo ilitokana na mabadiliko ya mwenendo wa mfumuko wa bei, ukuaji wa uchumi hususan kwenye mataifa yalioendelea, gharama za kukopa katika masoko ya fedha, na kuwepo kwa migogoro ya kisiasa.

Mwenendo wa uchumi wa Tanzania

Uchumi wa Tanzania ulitarajiwa kuendelea kuwa imara na stahimilivu kwa mwaka 2025. Mwenendo halisi ulishabihiana na matarajio, ambapo uchumi uliendelea kuwa imara na himilivu. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2025, ukishabihiana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, fedha na bima, pamoja na usafirishaji na uhifadhi. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 7, juu ya makadirio ya asilimia 6.5, ukiakisi uwekezaji mkubwa uliofanyika katika shughuli za utalii, ujenzi na viwanda.



Mfumuko wa bei ulitarajiwa kuendelea kuwa tulivu mwaka 2025/26, ambapo ulitarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Katika kipindi cha miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2025/26, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.4 kwa Tanzania Bara sawa na matarajio, ukichangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula. Aidha, viwango vya mfumuko wa bei vilikuwa ndani ya lengo la nchi na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya kikanda.

Mwenendo wa viwango vya riba, ujazi wa fedha, na mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha pamoja na kuimarika kwa mazingira ya ufanyaji biashara. Riba za mikopo katika benki za biashara zilipungua kidogo, wakati riba katika masoko ya fedha, hususan hati fungani na dhamana za Serikali, zilipungua kwa kiwango kikubwa. Aidha, Benki Kuu iliendelea kufanya maboresho yaliyolenga kuongeza ufanisi katika masoko ya fedha na kuboresha upatikanaji wa ukwasi, ili kuwezesha riba za benki za biashara kuendana na mwelekeo wa sera ya fedha. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuongeza wigo wa dhamana zinazokubalika kwa benki za biashara kukopa kutoka Benki Kuu na kuanza kutumika kwa mfumo unaoweka uwazi wa viwango vya riba na gharama mbalimbali zinazotozwa na benki (*Price Comparator System*) mwezi Desemba 2025. Ujazi wa fedha ulikua kwa wastani wa asilimia 22.4 katika miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2025/26, ukichangiwa na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, ambayo ilikuwa kwa asilimia 20.2.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika miezi tisa ya mwanzo ya 2025/26 ulikuwa wa kuridhisha. Mapato ya ndani ya Serikali ya Jamhuri ya



Muungano ya Tanzania yalizidi lengo kwa asilimia 5.5, kutokana na maboresho endelevu katika usimamizi wa kodi sambamba na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Kwa upande wa Zanzibar, utekelezaji wa bajeti ulikuwa pia wa kuridhisha ambapo mapato ya Serikali yalifikia asilimia 97.2 ya lengo. Deni la Serikali liliendelea kuwa himilivu, ambapo kiwango cha kiashiria cha uhatarishi kikibaki kuwa cha wastani. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2024/25, uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali (*present value*) kwa Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 40.7 kutoka asilimia 41.1 katika mwaka uliotangulia. Kiwango hiki ni chini ya ukomo wa uhimilivu wa deni wa asilimia 55.

Sekta ya nje iliendelea kuwa imara, ikichangiwa na ongezeko la mauzo nje ya nchi pamoja na idadi ya watalii wanaoingia nchini, sambamba na kasi ndogo ya ongezeko la uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Hata hivyo, kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia kuanzia mwezi Machi 2026, hususan mafuta ghafi na mbolea, kutokana na mgogoro wa Mashariki ya Kati kumeathiri urari wa malipo ya kawaida. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida, iliongezeka kidogo kufikia takriban asilimia 2.6 ya Pato la Taifa kwa mwaka unaoishia Machi 2026, ikilinganishwa na asilimia 2.4 kwa mwaka unaoishia Machi 2025. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha, ambapo ilifikia dola za Marekani milioni 5,722.5 mwezi Aprili 2026, kiasi kinachotosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa takriban miezi 4.4. Sambamba na uthabiti wa sekta ya nje, Shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu, ikiimarika dhidi ya dola ya Marekani kwa asilimia 2.7 kwa mwaka, ikilinganishwa na kushuka thamani kwa asilimia 3.9 mwishoni mwa Aprili 2025.

Sekta ya fedha iliendelea kuwa imara na thabiti. Sekta ya benki ilikuwa na mtaji, ukwasi wa kutosha, na yenye kutengeneza faida. Ubora wa



rasilimali za benki za biashara uliendelea kuimarika, kufuatia kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu (NPLs) hadi asilimia 2.9, ambao ni chini ya kiwango kinachohimilika cha asilimia 5.

Vilevile, kiwango cha ujumuishi wa fedha kimeendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za fedha kwa watu binafsi pamoja na biashara ndogo na za kati. Idadi ya wananchi wanaoweza kufikia huduma rasmi za fedha ndani ya umbali wa kilometa tano uliongezeka na kufikia asilimia 93.4. Wakati huohuo matumizi ya huduma za fedha kutoka katika taasisi za kibenki na zisizo za kibenki yaliongezeka katika kipindi kilichoishia Aprili 2026, sambamba na ongezeko la idadi ya akaunti binafsi kwa ajili ya amana na mikopo.

Mifumo ya malipo ilikuwa imara, ikiendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiwa na kiwango cha upatikanaji cha zaidi ya wastani wa asilimia 99.6. Benki Kuu iliendelea kuimarisha ufanisi na kuunganisha mifumo ya malipo na kuwezesha ufanyaji wa miamala ya moja kwa moja (*straight-through processing*) kwa malipo madogo na makubwa ndani na nje ya nchi. Aidha ongezeko kubwa limeonekana katika matumizi ya malipo ya kidijitali, kupitia miamala ya kifedha ya kielektroniki sambamba na kupungua kwa matumizi ya hundi.

Matarajio ya hali ya uchumi

Uchumi wa dunia

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026, inatarajiwa kupungua kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa nishati na kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa duniani. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuimarika kidogo mwaka 2027, ukiakisi matarajio ya kutengemaa kwa masoko ya nishati na fedha duniani.



Mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kuongezeka mwaka 2026, kutokana na kupanda kwa bei za nishati na bidhaa muhimu kwenye soko la dunia. Bei za nishati zinatarajiwa kuendelea kuongezeka mwaka 2026, kabla ya kuanza kupungua, kadri mnyororo wa ugavi utakavyoimarika na masoko ya fedha kutengemaa. Sambamba na matarajio ya ongezeko la mfumuko wa bei, benki kuu zinatarajiwa kuongeza au kutobadili viwango vya riba za sera ya fedha ili kudhibiti athari za mfumuko wa bei.

Uchumi wa ndani

Ukuaji wa uchumi wa ndani unatarajiwa kuendelea kuwa imara na thabiti kutokana na kutegemea sekta mbalimbali za uzalishaji, hivyo kusaidia kuhimili misukosuko kutoka nje ya nchi. Ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara unatarajiwa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026, na asilimia 6.6 mwaka 2027, ukichangiwa na ongezeko la uwekezaji wa serikali na sekta binafsi na mauzo nje ya nchi. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.5 mwaka 2026 na asilimia 7.2 mwaka 2027, ukichagizwa na shughuli za ujenzi, utalii na viwanda.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka, huku ukiendelea kubaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3 hadi 5. Kwa Tanzania Bara, mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa zaidi ya asilimia 4, wakati Zanzibar unatarajiwa kubaki karibu na asilimia 5. Hata hivyo, uwezekano wa mfumuko wa bei kuongezeka zaidi unategemea kwa kiasi kikubwa na muda na ukubwa wa mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati na athari zake kwa bei za nishati na bidhaa katika soko la dunia.



Sera ya fedha kwa 2026/27

Kwa kuzingatia matarajio ya mwenendo wa uchumi, sera ya fedha kwa mwaka 2026/27 italenga kupunguza ukwasi ili kudhibiti athari za kupanda kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia kwenye mfumuko wa bei wa ndani. Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) itaendelea kukutana kila baada ya robo mwaka kutathmini mwenendo wa uchumi na kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) ili kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo lililowekwa. Sambamba na hayo, utekelezaji wa sera ya fedha utaendelea kuhakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi ili riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki katika soko la fedha ibaki ndani ya wigo wa CBR.

Aidha, Benki Kuu, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kuhimiza na kuongeza kasi ya matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali, kuimarisha upatikanaji na ubora wa takwimu zinazohitajika katika kufanya maamuzi ya sera ya fedha, pamoja na kutoa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa kuhusu mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba. Hatua hizi zinalenga kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha.

Vilevile, Benki Kuu itaendelea kutekeleza maboresho katika sekta ya fedha kwa lengo la kuongeza ufanisi katika soko la fedha kati ya benki, kuimarisha usambazaji wa ukwasi katika mfumo wa kifedha, na kulinda utulivu wa sekta ya fedha. Aidha, ili kuimarisha uwezo wa sera ya fedha kukabiliana na mabadiliko ya mazingira ya uchumi wa ndani na wa dunia, kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni kitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko.



SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Tamko la Sera ya Fedha lililochapishwa mwezi Juni 2025, liliainisha mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26, baada ya kuzingatia matarajio ya uchumi wa dunia na wa hapa nchini, pamoja na vihatarishi vilivyokuwepo. Kutokana na matarajio ya mfumuko wa bei kubaki ndani ya lengo la wigo wa asilimia 3 hadi 5, Benki Kuu ilipanga kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi ili kuchagiza ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 6 kwa Tanzania Bara na asilimia 6.5 kwa Zanzibar, kwa mwaka 2025.

Tamko hili la Sera ya Fedha la mwaka 2026/27, linatathmini utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake kwa mwaka 2025/26, pamoja na mwenendo wa uchumi wa dunia na hapa nchini. Vilevile, Tamko hili linatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, na mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2026/27.

Pamoja na Sehemu hii ya Utangulizi, Tamko hili limepangwa kwa mtiririko ufuatao: Sehemu ya Pili inaainisha malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26. Sehemu ya Tatu inachambua mwenendo wa uchumi wa dunia, ikifuatiwa na Sehemu ya Nne inayotathmini mwenendo wa uchumi wa hapa nchini. Sehemu ya Tano inatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini na sehemu ya Sita inahitimisha kwa kutoa mwelekeo wa sera za fedha itakayotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2026/27 ili kufikia malengo yake.



Mfumo wa Sera ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania

Benki Kuu ya Tanzania ina jukumu la kuandaa na kutekeleza sera ya fedha, ikiwa ni moja kati ya majukumu yake. Malengo ya sera ya fedha ni kudumisha utulivu wa bei, ikimaanisha ni kuwa na mfumuko wa bei mdogo na usiobadilika mara kwa mara katika kipindi husika, pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi. Mfumuko wa bei hupimwa kwa kutumia badiliko la mwaka la Fahirisi za Bei za Walaji (CPI), na huwasilishwa kwa asilimia. Lengo la mfumuko wa bei la muda wa kati (hadi miaka 5), ni kati ya asilimia 3 hadi 5.

Ili kutimiza malengo haya, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) hutathmini mwenendo na matarajio ya uchumi na kuamua kiwango cha riba cha Benki Kuu (CBR) kinachoendana na mfumuko wa bei ulio chini na thabiti na kuweka mazingira ya kuchochea ukuaji wa uchumi. Benki Kuu ya Tanzania hutekeleza sera ya fedha kwa kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki ambayo ni kiashiria cha utekelezaji wa sera ya fedha kinakuwa ndani ya wigo wa CBR.

Ili kuoanisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabanki na CBR, Benki Kuu hutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha. Nyenzo hizi ni pamoja na mikopo ya muda mfupi (*repo na reverse repo*), dhamana za Serikali za siku 35 na 91, kuongeza au kupunguza kiwango cha amana kinachotakiwa kuweka kisheria na benki katika Benki Kuu (SMR), pamoja na mauzo au manunuzi ya fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni. Vilevile, Benki Kuu hutumia nyenzo nyingine ambazo ni mikopo ya siku moja na ile inayolipwa ndani ya siku husika, ambayo hutolewa kwa benki zenye uhitaji ili kuhakikisha kuwa mifumo ya malipo inafanya kazi kwa ufanisi.

Katika kutekeleza sera ya fedha, Benki Kuu huzingatia uwazi katika maamuzi yake. Maamuzi ya MPC, yakiwemo kuhusu riba ya Benki Kuu, huwasilishwa kwa benki kupitia mikutano ya Gavana na watendaji wakuu wa benki, na kwa umma kupitia vyombo vya habari. Aidha, Benki Kuu huchapisha matamko ya Kamati ya Sera ya fedha, Ripoti ya Sera ya Fedha, pamoja na ripoti nyingine ambazo huainisha matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha, mwelekeo wa sera ya fedha, maamuzi CBR na mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Ripoti hizi zinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania (www.bot.go.tz).



Msingi wa kisheria wa Sera ya Fedha

Mwanzo wa kila mwaka wa fedha, Benki Kuu ya Tanzania hutoa mwelekeo wa sera ya fedha katika Tamko lake la Sera ya Fedha kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.

Tamko la Sera ya Fedha huidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania na kuwasilishwa bungeni kupitia kwa Waziri anayesimamia masuala ya fedha kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Benki Kuu, Sura Na. 197.

Utaratibu huo pia unafuatwa wakati wa uandaaji wa Mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha, ambayo huainisha maendeleo ya utekelezaji wa sera ya fedha dhidi ya malengo yake, matarajio kwa kipindi cha mwaka kilichosalia, na hatua zitakazochukuliwa ili kufikia malengo ya sera.

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu, ambayo inaongozwa na Gavana, inawajibika kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kila robo mwaka, kuendana na malengo ya sera za uchumi za Serikali.

Kamati ya Ufuatiliaji na Uangalizi ya Menejimenti ya Benki Kuu inakutana kila siku kutathmini mwenendo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki (kiashiria cha uendeshaji) na kuamua hatua zitakazochukuliwa ili kuhakikisha riba hiyo inabaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu.



SEHEMU YA PILI

2.0 MSIMAMO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA

2.1 Msimamo wa Sera ya Fedha

Mwezi Juni mwaka 2025, Benki Kuu ilitoa Tamko la Sera ya Fedha ikibainisha kuwa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26 italenga kuongeza ukwasi ili kuwezesha ukuaji wa shughuli za kiuchumi, huku mfumuko wa bei nchini ukitarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Mwelekeo huu wa sera ya fedha ulitokana na matarajio ya kuendelea kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, upatikanaji wa chakula cha kutosha ndani ya nchi, na uthabiti wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha, licha ya uwepo wa mvutano wa kisiasa Mashariki ya Kati ulioathiri biashara na uwekezaji duniani.

2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha

Utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa ufanisi katika kuchagiza uimara na ustahimilivu wa uchumi, licha ya athari zilizotokana na mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati, hususan katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2025/26. Mwezi Julai 2025, Kamati ya Sera ya Fedha ilipunguza Riba ya Benki Kuu kutoka asilimia 6 hadi asilimia 5.75 kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2025, kufuatia matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya lengo, ikichangiwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, uthabiti wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni, na kuimarika kwa mazingira ya uchumi wa dunia.

Mwezi Oktoba 2025, Kamati ya Sera ya Fedha iliamua Riba ya Benki Kuu kubaki asilimia 5.75 kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2025, kutokana na matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya lengo, huku shughuli za kiuchumi zikiendelea kuimarika. Vilevile, Mwezi




Aprili 2026, Kamati ya Sera ya Fedha iliamua kutobadili Riba ya Benki Kuu kwa robo ya nne ya mwaka 2025/26, ikilenga kudhibiti mfumuko wa bei nchini dhidi ya athari za kuongezeka kwa mgogoro wa kisiasa Mashariki ya Kati inayoathiri uchumi wa dunia, kuvuruga mnyororo wa ugavi na kupelekea mabadiliko makubwa ya bei za bidhaa duniani.

Utekelezaji wa sera ya fedha umehakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, ukiakisiwa na riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki kubaki ndani ya wigo wa Riba ya Benki Kuu (Kielelezo 2.1a). Ili kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, Benki Kuu ilitumia nyenzo za sera ya fedha ikiwemo, kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki (*reverse repo*), kuuza dhamana za Serikali (za siku 35, 91 na 182), pamoja na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni. Kutokana na hatua hizo, amana za benki (*free reserves*) ndani ya Benki Kuu ziliongezeka ikiashiria kuimarika kwa ukwasi katika mfumo wa Benki (Kielelezo 2.1b). Kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha, mfumuko wa bei ulibaki ndani ya lengo, ukiwa wastani wa asilimia 3.4 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026. Vilevile, uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi ulisaidia kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi ambayo ilikua kwa wastani wa asilimia 20.2, na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi.




Kielelezo 2.1a: Riba ya Benki Kuu na Riba ya Mikopo ya Siku 7



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 2.1b: Amana za Benki



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Katika kuimarisha zaidi ufanisi wa sera ya fedha, na kuhakikisha malengo ya sera ya fedha yanafikiwa, Benki Kuu ilipunguza wigo wa riba ya Benki Kuu kwa asilimia 0.5 kuanzia mwezi Aprili 2026 na kuwa asilimia 1.5 juu au chini ya riba ya Benki Kuu. Sambamba na hilo, Benki ilifanya maboresho na kutoa mwongozo mpya wa dhamana zinazotakiwa kwa benki kuchukua mikopo ya muda mfupi kutoka Benki Kuu, ili kuongeza ufanisi katika mgawanyo wa ukwasi baina ya benki. Vilevile, Benki Kuu ilianza utekelezaji wa mfumo wa msaada wa dharura wa ukwasi (*Emergency Liquidity Assistance*) kwa benki zenye mitaji ya kutosha lakini zina changamoto ya ukwasi wa muda mfupi.



SEHEMU YA TATU

3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA

3.1 Mwenendo wa Shughuli za Uzalishaji

Uchumi wa dunia katika mwaka 2025, ulikabiliwa na changamoto zilizotokana na migogoro ya kisiasa, kuongezeka kwa ushuru wa forodha kwa baadhi ya nchi, na kutotabirika kwa sera za kiuchumi. Licha ya changamoto hizo, uchumi wa dunia ulikuwa stahimilivu, ukikua kwa asilimia 3.4 mwaka 2025 kwa mujibu wa makadirio ya Shirika la Fedha la Kimataifa (Jedwali 3.1)¹. Uthabiti huu umechangiwa na kuongezeka kwa mahitaji, utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuchagiza ukuaji wa uchumi, pamoja na uwekezaji katika teknolojia.

Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea uliendelea kuimarika mwaka 2025, ukikua kwa wastani na kutofautiana baina ya nchi na nchi, ukichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji pamoja na kupungua kwa mfumuko wa bei. Nchini Marekani, shughuli za kiuchumi ziliendelea kuwa imara, ingawa kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua ukilinganisha na mwaka 2024. Ukuaji wa uchumi kwa ukanda wa Ulaya, uliendelea kuimarika kadri mfumuko wa bei ulivyoendelea kupungua pamoja na kuongezeka matumizi ya walaji. Ukuaji katika uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi ulikuwa mkubwa kuliko makadirio ya awali, ukichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa sekta ya kilimo nchini Brazil, pamoja na ongezeko katika sekta ya huduma nchini India. Kasi ya ukuaji wa uchumi nchini China ilipungua, ikiakisi kushuka kwa mahitaji ya nje ya nchi na kutotabirika kwa hali ya biashara, licha ya kuimarika kwa uwekezaji katika matumizi teknolojia na sekta ya viwanda.

¹ Taarifa ya Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF World Economic Outlook*) ya Aprili 2026



Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi uliendelea kuwa imara na stahimilivu kwa mwaka 2025, ukichangiwa na kupungua kwa mfumuko wa bei katika baadhi ya nchi pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, ukanda huu unaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma katika soko la dunia, masharti magumu ya upatikanaji wa fedha kutoka nje, pamoja na mzigo wa madeni kwa baadhi ya nchi.

Jedwali 3.1: Ukuaji wa Pato la Taifa

Asilimia

	Halisi									Makadirio		
	Benki ya Dunia			Benki ya Dunia			Benki ya Dunia			Benki ya Dunia		
	IMF	OECD		IMF	OECD		IMF	OECD		IMF	OECD	
	2023			2024			2025			2026		
Dunia	3.0	2.9	2.1	3.3	3.2	2.7	3.4	3.1	2.7	3.3	2.9	2.4
Nchi zilizoendelea	1.5	n.a	0.7	1.8	n.a	1.7	1.9	n.a	1.7	1.8	n.a	1.4
Marekani	2.1	2.4	1.1	2.8	2.8	2.8	2.1	2.2	2.3	2.4	1.7	1.6
Eneo la Ulaya	0.7	0.6	1.3	0.9	0.7	0.7	1.4	1.0	1.0	1.3	1.2	0.8
Uingereza	0.5	n.a	n.a	1.1	0.9	n.a	1.3	1.4	n.a	1.3	1.2	n.a
Japani	2.0	1.7	0.8	0.1	0.1	0.0	1.2	1.1	0.9	0.7	0.9	0.8
Nchi zinazoibuka na Kuendelea Kiuchumi	4.0	n.a	4.0	4.3	n.a	4.1	4.4	n.a	4.1	4.2	n.a	3.8
Brazilii	3.0	3.0	1.2	3.4	3.4	3.2	2.3	2.1	2.2	1.6	1.7	2.2
Urusi	2.2	n.a	n.a	4.1	4.1	3.4	1.0	1.3	1.6	0.8	0.9	1.2
India	6.3	6.3	6.3	6.5	6.3	6.5	7.6	6.4	6.7	6.4	6.2	6.5
China	5.0	5.2	5.6	5.0	5.0	4.9	5.0	4.1	4.5	4.5	4.4	4.0
Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara	3.3	n.a	3.2	4.0	n.a	3.2	4.5	n.a	4.1	4.6	n.a	4.1

Chanzo : Ripoti ya IMF ya Mwelekeo wa Uchumi, Aprili 2026, Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu matarajio ya Uchumi wa Dunia ya Januari 2026; na Ripoti ya Mwelekeo wa Uchumi ya OECD, Machi 2026.

Tanbihi: n.a inaonyesha kukosekana kwa takwimu husika.

3.2 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei duniani ulitarajiwa kuendelea kupungua taratibu; ingawa kulikuwepo na vihatarishi vya kuweza kuongeza mfumuko wa bei kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya kibiashara na mivutano Mashariki ya Kati. Hivyo basi, benki kuu zilitarajiwa kuendelea kuchagiza ukuaji wa uchumi kwa kupunguza riba za sera ya fedha pale ilipohitajika. Mfumuko wa bei katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, ulikuwa kama ulivyotarajiwa, ambapo uliendelea kupungua kwa kasi tofauti baina ya nchi na nchi. Hata hivyo, mfumuko wa bei uliongezeka kuanzia Machi 2026, kufuatia mgogoro wa Mashariki ya Kati (Kielelezo 3.1a).



Hali hii ilisababisha ongezeko la mabadiliko ya bei katika masoko ya nishati duniani, na mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea, hususan Marekani na ukanda wa Ulaya.

Kwa upande wa nchi zinazoibukia kiuchumi, athari za mgogoro wa Mashariki ya Kati zilikuwa tofauti baina ya nchi. Nchini China, udhibiti wa bei za mafuta katika soko la ndani ulisaidia kupunguza mfumuko wa bei, wakati nchini India na Brazil mfumuko wa bei uliongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dhahabu na gharama za pembejeo za kilimo, mtawalia.

Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei uliendelea kubaki ndani ya malengo ya kitaifa na kikanda (Kielelezo 3.1b na 3.1c). Hata hivyo, kumekuwa na dalili za kuongezeka kwa mfumuko wa bei hususan katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kutokana na kupanda kwa bei za nishati sambamba na athari za kuongezeka kwa mfumuko wa bei duniani.



Kielelezo 3.1a: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizozendelea na Zinazoibukia Kiuchumi



Chanzo: Bloomberg

Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)



Kielelezo 3.1b: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)



Kielelezo 3.1c: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Mistari na nukta inaashiria lengo la mfumuko wa bei kwa nchi husika

3.3 Mwenendo wa Bei za Bidhaa

Matarajio ya mwenendo wa bei za bidhaa katika soko la dunia mwanzoni mwa mwaka 2026, yalikuwa tofauti baina ya bidhaa. Bei ya dhahabu ilitarajiwa kuongezeka, ikichangiwa na manunuzi ya benki kuu pamoja na ongezeko la mahitaji ya dhahabu kama hifadhi salama ya akiba. Wakati huohuo, bei ya mafuta ilitarajiwa kubaki katika viwango vya chini, kutokana na kupungua kwa mahitaji duniani na ongezeko la uzalishaji kutoka nchi za OPEC+. Hata hivyo, tofauti na matarajio ya awali, bei za bidhaa nyingi ziliongezeka kuanzia Machi 2026, tofauti na kipindi



cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26 ambapo zilipungua (Kielelezo 3.2a na 3.2b). Mabadiliko haya yalichochea kwa kiasi kikubwa na kuvurugika kwa ugavi kufuatia mivutano ya kisiasa Mashariki ya Kati.


Masoko ya nishati yaliathirika zaidi, ambapo bei ya mafuta ghafi iliongezeka hadi dola za Marekani 82.8 kwa pipa katika nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2025/26, ikilinganishwa na wastani wa dola 64.8 kwa pipa katika nusu ya kwanza ya mwaka. Aidha, bei ya juu zaidi ilifikia dola 137.8 kwa pipa mnamo tarehe 19 Machi 2026². Bei ya dhahabu ilipungua kidogo hadi dola za Marekani 4,855.5 kwa wakia moja mwezi Machi 2026, kutoka dola 5,020.0 kwa wakia moja mwezi Februari 2026. Mwenendo huu ulichangiwa na matarajio ya mabadiliko ya mwelekeo wa sera ya fedha ya Benki Kuu ya Marekani, hali iliyoimarisha thamani ya dola ya Marekani na kupunguza mahitaji ya dhahabu kama hifadhi salama ya akiba kwa wawekezaji.

Bei za mazao ya kilimo katika soko la dunia zilionesha mwenendo mchanganyiko. Bei za kahawa aina ya Arabika na Robusta zilipungua kiasi kufuatia kuongezeka kwa uzalishaji nchini Brazil katika msimu wa 2025/26, hali iliyosaidia kufidia upungufu wa uzalishaji katika maeneo mengine. Bei za bidhaa za chakula ziliongezeka, hususan bei za mafuta ya mawese, ngano, mchele na mahindi, kufuatia hali mbaya ya hewa katika maeneo ya uzalishaji, pamoja na kupanda kwa gharama za nishati na usafirishaji. Hali hii ilichangiwa pia na kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo hususan mbolea ya *Diammonium Phosphate* (DAP), kutokana na changamoto za ugavi na usafirishaji.

² Kiwango cha juu zaidi cha bei ya mafuta ghafi kilichotajwa, kinarejea bei ya mafuta ya Soko la Dubai ambapo shehena kubwa ya mafuta yanayoagizwa hapa nchini hutokea.




Kielelezo 3.2a: Bei za Baadhi ya Bidhaa katika Soko la Dunia



Chanzo: <http://www.worldbank.org/prospects>



Kielelezo 3.2b: Bei za Baadhi ya Bidhaa katika Soko la Dunia



Chanzo : <http://www.worldbank.org/prospects>

3.4 Mwenendo wa Masoko ya Fedha Duniani

Riba za hati fungani za serikali katika masoko ya fedha duniani kati ya Julai 2025 na Aprili 2026 zilikuwa na mienendo tofauti, zikichangiwa na mabadiliko ya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi, kuongezeka kwa ugumu wa upatikanaji wa fedha za bajeti za serikali, na athari za



kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa duniani. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, riba katika masoko ya fedha zilishuka kufuatia kupungua kwa riba za sera ya fedha, sambamba na kupungua kwa mfumuko wa bei. Hata hivyo, hali ya kutotabirika katika masoko ya fedha ilirejea mwanzoni mwa mwaka 2026 kufuatia kuongezeka kwa mivutano Mashariki ya Kati, hali iliyosababisha kupanda kwa bei za nishati, na kuibua hofu za ongezeko la mfumuko wa bei.

Nchini Marekani, riba za hati fungani za Serikali zilishuka kutokana na matarajio ya Benki Kuu ya Marekani kupunguza riba ya sera ya fedha. Hata hivyo, riba hizo zilipanda hasa kwa hati fungani za muda mrefu kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kupanda kwa bei ya mafuta ya nishati, na kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha za bajeti, hali iliyosababisha wawekezaji kutathmini upya matarajio yao kuhusu mwelekeo wa sera ya fedha.

Riba za hati fungani kwa ukanda wa Ulaya, zilishuka kwa ujumla, zikichangiwa na ukuaji mdogo wa uchumi na matarajio ya kupungua kwa riba ya sera ya fedha ya Benki Kuu ya Ulaya (ECB). Hata hivyo, kuongezeka kwa mfumuko wa bei unaotokana na kupanda kwa bei za nishati zilipunguza kasi ya kupungua zaidi kwa riba hizo. Nchini Uingereza, riba za hati fungani za Serikali zilishuka mwishoni mwa mwaka 2025 kabla ya kuanza kuongezeka katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, kutokana na hofu ya kuongezeka mfumuko wa bei wa ndani na ustahimilivu wa sera ya bajeti. Kwa upande wa China, riba za hati fungani za Serikali zilibaki katika viwango vya chini, zikisaidiwa na sera ya fedha ya kuongeza ukwasi, ingawa ongezeko dogo la riba lilionekana katika hati fungani za muda mrefu kutokana na matarajio ya mabadiliko ya masoko.



SEHEMU YA NNE

4.0 HALI YA UCHUMI NCHINI

4.1 Pato la Taifa


Mwezi Juni 2025, Benki Kuu ilitarajia uchumi kuendelea kuimarika, ambapo uchumi wa Tanzania Bara ulikadiriwa kukua kwa asilimia 6, huku uchumi wa Zanzibar ukitarajiwa kukua kwa asilimia 6.5. Mwenendo halisi ulishabihiana na matarajio, ambapo uchumi uliendelea kuwa imara na himilivu, licha ya changamoto mbalimbali za kiuchumi na kibiashara duniani.

Kwa upande wa Tanzania Bara, ukuaji wa Pato la Taifa ulifikia asilimia 5.9, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.6 mwaka 2024 (Kielelezo 4.1a). Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, fedha na bima, usafirishaji na uhifadhi, uchimbaji madini na mawe, pamoja na ujenzi (Kielelezo 4.1b). Aidha, mwenendo huu ulichagizwa na kuimarika kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika, kufuatia kuanza kwa uzalishaji wa umeme kutoka kituo cha kufua umeme wa maji cha Julius Nyerere, hali iliyochangia kuongeza tija katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Vilevile, kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na madini, utekelezaji wa miradi ya miundombinu, huduma za kijamii, pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma, vilichangia zaidi ukuaji wa uchumi.



Kielelezo 4.1a: Ukuaji wa Pato la Taifa


Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 4.1b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu



Uchumi wa Zanzibar uliendelea kuwa imara, ukikua kwa asilimia 7 mwaka 2025, juu ya matarajio ya ukuaji wa asilimia 6.5, japo ulikuwa chini kidogo ya ukuaji wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2024 (Kielelezo 4.2a). Ukuaji huu ulichagizwa na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo bandari, barabara na miundombinu mingine. Aidha, ukuaji huu uliakisi pia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali na sekta binafsi katika sekta ya utalii. Shughuli nyingine zilizochangia ukuaji huu ni pamoja na; mifugo, ujenzi, viwanda, na kilimo (Kielelezo 4.2b).

Kielelezo 4.2a: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Zanzibar




Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar



Kielelezo 4.2b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

4.2 Mfumuko wa Bei


Mfumuko wa bei ulikuwa sawa na matarajio, ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 ulibaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Mfumuko wa bei wa Tanzania Bara ulikuwa wastani wa asilimia 3.4, ukiwa ndani ya lengo la kitaifa na kukidhi vigezo vya mtangamano vya kikanda vya SADC na EAC (Kielelezo 4.3a na 4.3b). Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula. Hata hivyo, mwezi Aprili 2026, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 4, ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kufikiwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kutokana na kupanda kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia, kufuatia mgogoro wa Mashariki ya Kati. Ongezeko hilo la bei za mafuta katika soko la dunia limeathiri pia sekta nyingine za uchumi kupitia ongezeko la gharama za usafirishaji na bei za mafuta nchini. Serikali imechukua



hatua kadhaa kwa ajili ya kukabiliana na mfumuko wa bei, ikiwemo kutoa ruzuku ya mafuta ya dizeli pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa masoko ili kuhakikisha gharama za usafiri zinaendelea kuwa nafuu kwa wananchi.

Mfumuko wa bei wa msingi (*core inflation*), ambao huchangia takriban asilimia 73.9 ya kapu la bidhaa na huduma za mlaji, uliendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa mfumuko wa bei wa jumla kwa takriban asilimia 2.4 (Kielelezo 4.3c). Ongezeko hili linatokana zaidi na kupanda kwa bei za huduma na chakula kilichochakatwa. Aidha, mfumuko wa bei za chakula, hususan chakula kisichochakatwa, uliongezeka hadi wastani wa asilimia 7.4 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, kutoka wastani wa asilimia 2.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 ukichangiwa na changamoto za upatikanaji wa baadhi ya bidhaa za chakula.

Kielelezo 4.3a: Mfumuko wa Bei




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu



Kielelezo 4.3b: Mfumuko wa Bei na Malengo ya Nchi na Kikanda


Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kielelezo 4.3c: Mchango katika Mfumuko wa Bei

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu



Mfumuko wa bei wa Zanzibar, ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, ikilinganishwa na asilimia 5 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula pamoja na bidhaa zisizo za chakula (Kielelezo 4.4). Mfumuko wa bei wa chakula ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 7.1, hali iliyochangiwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani sambamba na juhudi za Serikali za kudhibiti ongezeko la bei za chakula. Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula ulipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 2 kutoka asilimia 3.4 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kupungua mfumuko wa bei katika kundi la bidhaa zisizo za chakula kulitokana na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za mavazi na viatu.

Kielelezo 4.4: Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar



Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar



4.3 Viwango vya Riba

Katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2025/26, riba za muda mfupi katika soko la fedha ziliendelea kuakisi mwelekeo wa sera ya fedha, isipokuwa zile za muda mrefu, hali inayoashiria uwepo wa changamoto za kimfumo. Riba za dhamana za Serikali za muda mfupi ziliendelea kupungua hadi wastani wa asilimia 6.12, kutoka asilimia 11.08 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25, sanjari na ongezeko la mahitaji ya uwekezaji katika dhamana za Serikali na ukwasi wa kutosha (Kielelezo 4.5a). Riba za mikopo zilipungua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 15.18 kutoka asilimia 15.47, huku riba za mikopo inayotolewa kwa wateja wakubwa zikifikia asilimia 12.47 kutoka asilimia 12.91. Aidha, riba za amana zilikuwa wastani wa asilimia 8.47, huku riba za amana kwa wateja wakubwa zikifikia asilimia 11.35 (Kielelezo 4.5b).


Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliendelea kutekeleza maboresho yaliyolenga kupunguza vihatarishi vya mikopo na kuongeza ufanisi wa soko la fedha ili kuwezesha riba za benki kuendana na mwelekeo wa sera ya fedha. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kupanua wigo wa dhamana zinazokubalika katika utoaji wa mikopo, pamoja na uanzishwaji wa mfumo wa ulinganishi wa bei (*Price Comparator*) mwezi Desemba 2025³. Mfumo huu unatarajiwa kuongeza uwazi wa riba zinazotozwa na benki mbalimbali na hivyo kuwasaidia wakopaji kufanya maamuzi sahihi na kuongeza ushindani katika sekta ya benki⁴.

³ Mfumo unaowawezesha wateja wa huduma za fedha kulinganisha ada, viwango vya riba, na gharama nyingine baina ya taasisi za fedha zilizosajiliwa nchini Tanzania.

⁴ Benki Kuu pia imeendelea kufuatilia utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa vipindi vya nyuma ikiwemo kuhamasisha matumizi ya taarifa kutoka katika kanzidata ya taarifa za wakopaji, na kuimarisha mifumo ya kulinda watumiaji pamoja na utekelezaji wa programu za elimu ya fedha na juhudi za kuongeza ujumuishi wa kifedha




Kielelezo 4.5a: Riba katika Masoko ya Fedha



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.5b: Riba za Amana na Mikopo Inayotolewa Benki za Biashara




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



4.4 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi

Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa mwaka 2025/26, uliendelea kuakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi katika uchumi. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 22.4 katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2025/26 (Kielelezo 4.6a na 4.6b). Ukuaji huo ulichochea zaidi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, sanjari na kuimarika kwa mazingira ya uchumi na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha kwa ajili ya uwekezaji na shughuli za uzalishaji.


Kielelezo 4.6a: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Kielelezo 4.6b: Mchango katika Ukuaji wa Ujazi wa Fedha (M3)




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 20.2. Mwenendo huu ulichagizwa na utekelezaji wa hatua za kisera zilizolenga kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu, ikiwemo mifuko ya dhamana za mikopo na mkopo maalumu wa shilingi trilioni moja iliyoelekezwa katika sekta ya kilimo, pamoja na nafuu inayotolewa kwa amana zinazotakiwa kuwekwa na benki katika Benki Kuu kwa ajili ya mikopo inayotolewa kwenye shughuli za kilimo. Mwenendo huu wa ukuaji wa mikopo unaakisi pia utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti sambamba na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Mchango wa huduma za fedha katika uchumi umeendelea kuimarika ukiakisiwa na ongezeko la uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi dhidi ya Pato la Taifa (GDP), ambao ulifikia asilimia 23.2 mwezi Aprili 2026, kutoka asilimia 18.7 kwa kipindi kama hicho 2025.



Aidha, hakukuwa na mabadiliko makubwa katika mchanganuo wa mikopo kwa sekta binafsi, ambapo shughuli binafsi za uzalishaji ziliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote kwa sekta binafsi (Kielelezo 4.7a na 4.7b). Mwenendo wa mikopo kwa sekta ya kilimo uliendelea kuwa wa kuridhisha, ukiwa na ukuaji wa asilimia 30.5 na mchango katika ukuaji wa mikopo wa asilimia 17.2.


Kielelezo 4.7a: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Ukuaji wa Mikopo, kwa Asilimia



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Kielelezo 4.7b: Mgawanyo wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi, kwa Asilimia



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Katika miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2025/26, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliendelea kutekeleza bajeti kwa ufanisi huku ikipanga matumizi kulingana na rasilimali zilizopo. Katika kipindi hiki, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 31,406.1, yakivuka lengo kwa asilimia 5.5 (Jedwali 4.1). Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 26,037.6, zaidi ya makadirio kwa asilimia 9.4, ikichangiwa na maboresho katika usimamizi wa kodi na utayari wa kulipa kodi kwa hiyari. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 4,145.3, sawa na asilimia 88.2 ya lengo. Wakati huohuo, matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 35,334.9, ambapo asilimia 35.1 ilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo, sambamba na jitihada za Serikali katika kuelekeza rasilimali za umma kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayolenga kuimarisha miundombinu, kuongeza uzalishaji na kuchochea ukuaji wa uchumi.



Jedwali 4.1 Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Tanzania Bara (Julai – Machi).

Shilingi Bilioni

	2024/25		2025/26	
	Halisi	Makisio	Halisi	Halisi/Makisio (%)
Mapato	25,669.8	29,776.2	31,406.1	105.5
Matumizi	31,238.1	36,263.7	35,334.9	97.4
Matumizi ya Kawaida	19,765.1	22,903.2	22,928.5	100.1
Matumizi ya Maendeleo	11,473.0	13,360.5	12,406.4	92.9


Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar uliendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mapato ya Serikali pamoja na misaada yalifikia shilingi bilioni 1,770, sawa na asilimia 97.2 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa asilimia 91.2, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni misaada. Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 1,462.1, sawa na asilimia 97.2 ya lengo, ambapo makundi yote ya kodi yalionyesha mwenendo wa kuridhisha. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 152.1, sawa na asilimia 74.3 ya lengo (Kielelezo 4.8a). Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 3,196.9, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 1,437.1 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 1,759.9 (Kielelezo 4.8b). Fedha za ndani zilichangia asilimia 80.5 ya matumizi ya maendeleo, hali inayoakisi dhamira ya Serikali katika kuimarisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miundombinu ya kiuchumi na kijamii, huku sehemu iliyobaki ikitokana na vyanzo vya nje.



Kielelezo 4.8a: Mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar


Shilingi Bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

Kielelezo 4.8b: Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

Shilingi Bilioni



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar



4.6 Deni la Taifa

Deni la Serikali liliendelea kuwa himilivu, huku kiwango cha kiashiria cha uhatarishi kikibaki kuwa cha wastani. Uwiano wa deni la Serikali kwa thamani ya sasa kwa Pato la Taifa (GDP) ulikuwa asilimia 40.7 mwaka 2024/25, ikilinganishwa na asilimia 41.1 mwaka uliotangulia na chini ya ukomo wa uhimilivu wa asilimia 55.

Kwa bei za sasa, deni la Serikali lilifikia dola za Marekani milioni 44,835.1 mwishoni mwa Aprili 2026 sawa na asilimia 47.7 ya Pato la Taifa. Kiwango hiki ni ndani ya kiwango cha ukomo wa mtangamano wa jumuiya ya SADC cha asilimia 60 (Jedwali 4.2a). Kati ya deni lote, deni la nje lilikuwa asilimia 66.3, ambapo kiasi kikubwa ilikuwa ni mikopo nafuu kutoka mashirika ya kimataifa, ikifuatiwa na mikopo ya biashara. Sehemu kubwa ya fedha za mikopo zilizopokelewa zilielekezwa kwenye kugharamia miradi ya usafirishaji na mawasiliano, ikifuatiwa na mahitaji ya kugharamia urari wa malipo ya nje, bajeti ya serikali pamoja na shughuli za ustawi wa jamii na elimu. Deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 39,335.8 mwezi Aprili 2026, likiwa ni ongezeko la asilimia 3.8 ikilinganishwa na kiwango kilichokuwepo mwishoni mwa Disemba 2025. Hati fungani za Serikali zimeendelea kuchukua sehemu kubwa ya deni la ndani (Jedwali 4.2b). Kwa upande wa Zanzibar, deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 2,704.9 mwezi Aprili 2026, likichangiwa zaidi na uwekezaji katika hati fungani za Serikali pamoja na mikopo kutoka benki za biashara.



Jedwali 4.2a: Mwenendo wa Deni

Dola za Marekani Milioni

	Jun-25	Dec-25 ^r	Apr-26 ^a
Deni la Serikali Kuu	41,874.7	44,812.3	44,835.1
Deni la nje	28,243.6	29,327.3	29,717.5
Jumla ya deni la Serikali (Asilimia)	67.4	65.4	66.3
Deni la ndani	13,631.1	15,485.0	15,117.6
Deni la nje la sekta binafsi	6,517.9	6,201.5	6,232.1
Deni la nje la mashirika ya umma	3.8	3.8	0.0
Jumla ya deni la nje	34,765.3	35,528.8	35,949.6
Jumla ya deni la Taifa	48,396.3	51,013.8	51,067.2

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na a, takwimu za awali

Jedwali 4.2b: Deni la Ndani la Serikali

Shilingi Bilioni

Nyenzo	Jun-25		Des-25		Apr -26 ^a	
	Kiasi	Asilimia	Kiasi	Asilimia	Kiasi	Asilimia
Dhamana za serikali	30,170.4	85.0	33,012.5	87.1	33,438.1	85.0
Dhamana za serikali za muda mfupi	2,001.3	5.6	1,951.9	5.2	1,518.7	3.9
Hisa za serikali	187.1	0.5	135.7	0.4	135.7	0.3
Dhamana za serikali za muda mrefu	27,982.0	78.8	30,924.8	81.6	31,783.7	80.8
Vyeti vya ushuru	0.1	0.0	0.1	0.0	0.1	0.0
Deni lisilo na dhamana	5,332.4	15.0	4,886.5	12.9	5,897.6	15.0
Madeni mengine*	18.4	0.1	0.0	0.0	0.0	0.0
Bakaa hasi	5,314.0	15.0	4,886.5	12.9	5,897.6	15.0
Deni la ndani (ukiondoa Dhamana za Benki Kuu)	35,502.8	100.0	37,899.0	100.0	39,335.8	100.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: * inajumuisha mkopo wa kawaida wa NMB; a, inamaanisha takwimu za awali

4.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliendelea kuwa thabiti, licha ya madhara yaliyotokana na vita ya Ukraine na kutotabirika kwa sera za biashara duniani. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025/26, urari wa malipo ya kawaida uliimarika, ukichagizwa na ongezeko la mauzo ya mazao ya kilimo, dhahabu, na mapato ya utalii sambamba na kasi ndogo ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi. Hata hivyo, kwa kipindi cha nusu ya



pili ya mwaka 2025/26, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilianza kuongezeka, ikichangiwa na mgogoro wa kisiasa Mashariki ya Kati.

Katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2025/26, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 2,027.2, kutoka dola za Marekani milioni 1,544.1 mwaka uliopita, ikichangiwa na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa nje ya nchi, ikiwemo mashine na mitambo, vyombo vya usafiri na malighafi za viwandani (Jedwali 4.3 na Kielelezo 4.9). Ingawa ongezeko la uagizaji wa bidhaa za mtaji na pembejeo za uzalishaji linaweza kuongeza nakisi ya urari wa malipo ya kawaida katika kipindi cha muda mfupi, mwenendo huo unaashiria kuimarika kwa shughuli za uzalishaji na uwekezaji katika uchumi katika kipindi cha muda mrefu. Katika mwaka ulioishia Aprili 2026, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilikuwa dola milioni 2,650.8 (asilimia 2.6 ya Pato la Taifa) ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,112.1 (asilimia 2.4 ya Pato la Taifa) kwa mwaka ulioishia Aprili 2025.

Jedwali 4.3: Urari wa Malipo ya Kawaida

	<i>Dola Milioni</i>					
	Mwaka ulioishia Aprili				Julai - Aprili	
	2022	2024	2025	2026 ^a	2024/25	2025/26 ^a
Urari wa Bidhaa (halisi)	-7,159.1	-5,979.9	-4,553.6	-5,353.5	-3,585.7	-4,344.9
Zilizouzwa nje*	7,246.3	7,815.8	9,682.7	11,215.0	8,407.2	9,750.6
Zilizonunuliwa nje	-14,405.5	-13,795.7	-14,236.3	-16,568.5	-11,992.9	-14,095.5
Urari wa Huduma (halisi)	2,586.7	4,151.4	3,908.0	4,285.6	3,293.8	3,627.9
Mapato	5,237.3	6,466.0	6,942.3	7,661.7	5,940.9	6,487.2
Malipo	-2,650.6	-2,314.6	-3,034.2	-3,376.1	-2,647.1	-2,859.3
Urari wa Bidhaa na Huduma (halisi)	-4,572.4	-1,828.5	-645.6	-1,067.9	-291.9	-717.0
Bidhaa na Huduma zilizouzwa nje	12,483.6	14,281.7	16,625.0	18,876.7	14,348.1	16,237.8
Bidhaa na Huduma zilizonunuliwa kutoka nje	-17,056.0	-16,110.2	-17,270.5	-19,944.6	-14,640.0	-16,954.8
Urari wa mapato ya vitega uchumi (halisi)	-1,458.7	-1,608.4	-1,998.4	-1,851.0	-1,669.0	-1,508.6
Yaliyoingia	189.3	338.5	301.8	298.7	253.2	259.8
Yaliyotoka	-1,648.0	-1,946.9	-2,300.2	-2,149.7	-1,922.2	-1,768.4
Urari wa Uhamisho Mali ya kawaida (halisi)	591.1	667.8	531.9	268.1	416.8	198.4
Iliyoingia	823.3	1,323.6	1,117.2	926.4	902.3	768.3
ambapo Serikalini	63.2	140.9	133.1	20.2	96.2	12.7
Iliyoingia	-232.2	-655.8	-585.3	-658.3	-485.5	-570.0
Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mapato	-5,440.0	-2,769.1	-2,112.1	-2,650.8	-1,544.1	-2,027.2


Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: a, inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebesho kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yasiyorekodiwa



Kielelezo 4.9: Urari wa Malipo ya Kawaida

Dola Milioni



Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebisho kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yasiyorekodiwa

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 16,237.8, katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2025/26, ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.2 kutoka dola milioni 14,348.1 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/25. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, mapato ya utalii, mauzo ya bidhaa za viwandani na bidhaa za kilimo kama vile tumbaku, korosho na kahawa (Jedwali 4.4 na Kielelezo 4.10). Dhahabu na utalii vimechangia kiasi kikubwa cha mauzo ya nje ya nchi, kwa pamoja vikichangia asilimia 51.3 ya mauzo yote ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Kwa mwaka ulioishia Aprili 2026, mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 18,876.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 16,625 kwa mwaka ulioishia Aprili 2025.



Jedwali 4.4: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi


Dola Milioni

	Mwaka ulioishia Aprili			Julai - Aprili	
	2024	2025	2026 ^a	2024/25	2025/26 ^a
Bidhaa Asilia	1,051.7	1,459.0	1,625.9	1,394.0	1,579.6
Bidhaa Zisizo Asilia	6,362.6	7,821.9	9,271.9	6,669.2	7,887.5
ambapo Dhahabu	3,133.3	3,821.2	5,268.9	3,292.1	4,511.9
Bidhaa za Viwandani	1,359.6	1,389.9	1,897.2	1,200.6	1,620.0
Mazao ya Mboga na Maua	411.3	514.4	466.5	478.3	436.6
Mapato ya Huduma	6,466.0	6,942.3	7,661.7	5,940.9	6,487.2
ambapo Utalii	3,589.9	4,006.3	4,385.3	3,443.7	3,732.5
Usafirishaji	2,296.0	2,419.3	2,834.8	2,077.6	2,374.1
Mauzo ya Bidhaa na Huduma	14,281.7	16,625.0	18,876.7	14,348.1	16,237.8

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a inamaanisha takwimu za awali

Kielelezo 4.10: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

Dola Milioni



Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a inamaanisha takwimu za awali



Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ulifikia dola za Marekani milioni 16,954.8 katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 15 kutoka dola za Marekani milioni 14,640 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (Jedwali 4.6). Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na uagizaji wa mashine na mitambo, vifaa vya usafiri kwa matumizi ya viwanda na malighafi za viwandani, vikiakisi uwekezaji katika miundombinu na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji viwandani. Uagizaji wa bidhaa za petroli ambazo zilichangia asilimia 14 ya uagizaji wa bidhaa zote, uliongezeka kwa asilimia 2.4 na kufikia dola za Marekani milioni 2,105.6. Ongezeko hili linaakisi mwenendo wa bei katika soko la dunia. Aidha, malipo ya huduma za usafirishaji wa bidhaa yaliongezeka sambamba na ongezeko la uagizaji wa bidhaa. Katika mwaka ulioishia Aprili 2026, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje ya nchi ilifikia dola za Marekani milioni 19,944.6, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 17,270.5 kwa mwaka ulioishia Aprili 2025.

Jedwali 4.5: Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

	<i>Dola Milioni</i>					
	Mwaka ulioishia Aprili			Julai - Aprili		
	2024	2025	2026 ^a	2024/25	2025/26 ^a	
Bidhaa za kukuza mtaji	2,909.1	2,929.4	4,132.7	2,506.2	3,577.3	
Bidhaa za kati	9,439.8	9,874.3	10,842.5	8,291.7	9,200.6	
Malighafi za viwanda	4,375.5	4,873.8	5,753.6	4,157.6	4,836.6	
Mafula na vilainishi	2,904.7	2,660.8	2,519.6	2,155.9	2,207.2	
ambapo Bidhaa za petroli zilizochujwa	2,684.5	2,506.3	2,415.8	2,055.3	2,105.6	
Vifaa	977.7	1,115.2	1,199.3	957.0	1,008.6	
Bidhaa za matumizi ya kawaida	1,444.6	1,430.5	1,591.0	1,193.1	1,315.6	
Malipo ya huduma	2,314.6	3,034.2	3,376.1	2,647.1	2,859.3	
ambapo Usafirishaji	1,276.2	1,426.5	1,666.2	1,228.4	1,427.3	
Utalii	370.8	643.1	702.2	572.8	606.1	
Huduma nyinginezo	667.6	964.6	1,007.7	846.0	825.9	
Malipo ya bidhaa na huduma	16,110.2	17,270.5	19,944.5	14,639.3	16,954.0	

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: ^a inamaanisha takwimu za awali



Urari wa malipo ya kawaida kwa Zanzibar uliongezeka kwa asilimia 24.9 na kufikia dola za Marekani milioni 795.2 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, kutoka dola za Marekani milioni 638.9 katika kipindi hicho mwaka 2024/25. Mwenendo huu unaakisi ongezeko la mapato yatokanayo na huduma (Jedwali 4.7). Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 46, yakichangiwa zaidi na kuimarika kwa mapato ya huduma, hususan shughuli za utalii. Vilevile, uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 57.4 na kufikia dola za Marekani milioni 694.7, hususan kutokana na ongezeko la uagizaji wa vifaa vya usafiri kwa matumizi ya viwandani, bidhaa za chakula pamoja na mashine (Jedwali 4.6, 4.7a na 4.7b).

Jedwali 4.6: Urari wa Malipo ya Kawaida kwa Zanzibar

Dola Milioni

Bidhaa	Mwaka unaoishia Aprili			Julai - Aprili	
	2024	2025	2026	2024/25	2025/26 ^a
Urari wa bidhaa	-434.0	-492.6	-613.1	-418.9	-528.1
Zilizouzwa nje	64.6	33.8	64.1	30.1	60.9
Zilizonunuliwa nje	498.6	526.4	677.2	449.0	589.0
Urari wa huduma	888.1	1,187.5	1,432.3	914.9	1,316.4
Mapato	985.7	1,287.7	1,553.8	985.7	1,422.1
Malipo	97.6	100.2	121.5	70.8	105.7
Urari wa Bidhaa na Huduma	454.1	694.9	819.1	496.0	788.3
Bidhaa na Huduma zilizouzwa nje	1,050.4	1,321.5	1,617.9	1,015.9	1,483.0
Bidhaa na Huduma zilizonunuliwa kutoka nje	596.3	626.6	798.7	519.8	694.7
Urari wa mapato ya vitega uchumi	12.1	13.7	7.6	99.5	6.1
Yaliyoingia	17.7	19.7	9.2	118.7	7.5
Yaliyotoka	5.6	6.0	1.7	19.2	1.4
Urari wa uhamisho mali ya kawaida	1.7	1.7	1.1	43.4	0.8
Iliyoingia	3.0	3.3	1.7	52.2	1.3
Iliyotoka	1.2	1.6	0.6	8.8	0.5
Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	467.9	710.2	827.8	638.9	795.2

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a inamaanisha takwimu za awali



Jedwali 4.7a: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi kwa Zanzibar

Dola milioni

	Mwaka unaoishia Aprili			Julai - Aprili	
	2024	2025	2026	2024/25	2025/26 ^a
Bidhaa asilia					
Karafuu	28.8	3.3	38.7	3.2	38.4
Bidhaa zisizo asilia					
Mwani	6.9	3.7	1.4	2.7	0.9
Bidhaa za viwandani	18.9	14.7	11.1	13.8	9.5
Samaki na bidhaa zitokanazo na samaki	2.1	1.6	0.6	1.1	0.6
Bidhaa nyinginezo	7.9	10.5	12.2	9.4	11.6
Jumla	35.9	30.4	25.4	26.9	22.5
Jumla kuu	64.6	33.8	64.1	30.1	60.9

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: a inamaanisha takwimu za awali

Jedwali 4.7b: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nje ya Nchi kwa Zanzibar

Dola Milioni

	Mwaka unaoishia Aprili			Julai - Aprili	
	2024	2025	2026	2024/25	2025/26 ^a
Bidhaa za kukuza mtaji	68.7	66.1	172.5	59.9	163.5
Bidhaa za kati	371.6	391.2	404.6	330.7	336.2
Mafuta na vilainishi	179.4	159.1	107.8	58.4	89.4
ambapo Bidhaa za petroli iliyochojwa	179.3	157.5	107.8	132.1	81.1
Bidhaa za matumizi ya viwandani	93.9	118.8	188.8	101.3	166.9
Vipuri na aksesori	13.6	16.3	31.0	13.8	28.7
Bidhaa za matumizi ya kawaida	58.3	69.1	100.1	58.4	89.4
Chakula na vinywaji kwa matumizi ya kawaida	13.7	17.3	18.6	14.6	16.0
Vifaa vya usafiri wa kawaida	1.9	2.2	3.0	2.0	1.2
Bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida	42.7	49.5	74.2	1.2	1.7
ambapo Bidhaa za dawa	1.5	3.7	1.7	3.6	1.0
Jumla	498.6	526.4	677.2	449.0	589.0

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: a inamaanisha takwimu za awali



4.8 Ukwasi wa Fedha za Kigeni, Thamani ya Shilingi na Akiba ya Fedha za Kigeni


Soko la fedha za kigeni liliendelea kuwa tulivu na ukwasi wa kutosha kwa mwaka 2025/26, ikichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii, mauzo ya dhahabu kufuatia bei nzuri katika soko la dunia, pamoja na mazao ya kilimo. Ukwasi wa fedha za kigeni uliendelea kuakisi mwenendo wa bei za bidhaa katika soko la dunia, matarajio ya soko na mapato ya fedha za kigeni.

Thamani ya shilingi ya Tanzania iliimarika dhidi ya dola ya Marekani, ikichangiwa na kuimarika kwa mwenendo wa uchumi, kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni na kupungua kwa mahitaji katika soko. Katika kipindi kilichoishia Aprili 2026, shilingi iliimarika kwa wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka, ikilinganishwa na kupungua kwa thamani kwa asilimia 3.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Vilevile, kiwango cha ubadilishaji fedha katika soko la rejareja kiliendelea kuwa karibu na viwango vya ubadilishaji fedha katika soko la fedha za kigeni baina ya benki, hali inayoashiria kuimarika kwa ufanisi wa soko na hivyo kuondoa mazingira ya uwepo soko lisilo rasmi la fedha za kigeni (Kielelezo 4.11a).

Kiwango halisi cha ubadilishaji fedha za kigeni kinachozingatia uwiano wa biashara baina ya Tanzania na washirika wa biashara (*Real Effective Exchange Rate-REER*) kiliendelea kuendana na hali ya kiuchumi, hivyo kuashiria kuendelea kuwepo kwa ushindani wa biashara nje ya nchi (Kielelezo 4.11b).




Kielelezo 4.11a: Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kielelezo 4.11b: Kiwango Halisi cha Ubadilishaji wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha katika kipindi chote cha miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2025/26 ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuendelea kwa utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa dhahabu kutoka ndani ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,722.5 mwishoni mwa mwezi Aprili 2026, kiasi kinachotosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 4.4 (Kielelezo 4.12a na 4.12b). Akiba hii ilikuwa juu ya lengo la nchi la miezi 4 na karibu na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za EAC cha miezi 4.5.


Kielezo 4.12a: Akiba ya Fedha za Kigeni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Kielelezo 4.12b: Miezi ya Uagizaji wa Bidhaa na Huduma



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha iliendelea kuwa thabiti, ikiwa na viwango vya chini vya vihatarishi, ikisaidiwa na utulivu wa uchumi. Sekta ya benki ambayo huchukua sehemu kubwa ya sekta ya fedha iliendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha, na yenye kutengeneza faida. Rasilimali za benki ziliongezeka sambamba na amana, zikichochea na ongezeko la huduma za uwakala wa benki, pamoja na utoaji wa huduma za kibenki kutumia mifumo ya kidijitali. Ubora wa rasilimali uliendelea kuimarika ambapo mikopo chechefu ilipungua hadi asilimia 2.9 mnamo Aprili 2026 kutoka asilimia 3.3 mwezi Juni 2025, ikiwa chini ya ukomo unaostahimilika na Benki Kuu wa asilimia 5. Kiwango hiki kinategemewa kuendelea kupungua kadri benki zinavyoendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza ubora wa rasilimali zao. Wakati huohuo, ukwasi katika



mfumo wa kibenki ulikuwa wa kutosha, ambapo uwiano wa rasilimali zinazoweza kukidhi mahitaji ya fedha ya muda mfupi (*Liquidity Coverage Ratio*) ulikuwa juu ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 100.

Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuimarisha sekta ya fedha. Hatua hizi ni pamoja na (i) kutoa miongozo ya usalama wa huduma za kidijitali, (ii) kuandaa mfumo wa kikanuni na usimamizi kwa ajili ya huduma za benki zisizo na riba (*Islamic Banking*) na (iii) kukusanya takwimu papo kwa papo kutoka benki na taasisi za fedha ili kuboresha usimamizi wa sekta hii na hivyo kuiwezesha Benki Kuu kuchukua hatua za kiusimamizi. Maboresho haya pia yanalenga kuwezesha wananchi kufikia na kutumia huduma mbalimbali za kifedha.

Aidha, kiwango cha ujumuishi wa fedha kimeendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za fedha kwa watu binafsi pamoja na biashara ndogo na za kati. Upatikanaji wa huduma rasmi za fedha kwa wananchi ndani ya umbali wa kilomita tano uliongezeka hadi asilimia 93.4. Vilevile, matumizi ya huduma za fedha kutoka katika taasisi za kibenki na zisizo za kibenki yaliongezeka katika kipindi kilichoishia Aprili 2026, ambapo idadi ya akaunti binafsi kwa ajili ya amana na mikopo ziliongezeka.

4.10 Mifumo ya Malipo

Mifumo ya malipo ya Taifa iliendelea kuwa thabiti, yenye ufanisi, na kupatikana kwa zaidi ya wastani wa asilimia 99.6, katika kipindi chote cha miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2025/26. Benki Kuu imeendelea kuboresha mifumo ya malipo, kwa kutekeleza awamu ya tatu ya Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo (*Tanzania Instant Payment System-TIPS*) unaolenga kuongeza wigo wa huduma zinazotolewa kupitia mfumo



huo, kuongeza ufanisi wa mfumo wa uhamishaji wa fedha kwa kuhamia kwenye viwango vya kimataifa vya jumbe za miamala vya ISO 20022. Hatua hizi zitaongeza ufanisi, kuaminika, na mwingiliano wa mifumo ya ndani na ile ya kimataifa.


Katika jitihada za kuongeza matumizi ya malipo ya mifumo ya kidijitali na kupunguza utegemezi wa matumizi ya fedha taslimu, Benki Kuu iliweka ukomo wa gharama za kutuma fedha kupitia mfumo wa malipo ya Papo kwa Papo (TIPS) baina ya benki na mitandao ya simu za mkononi. Vilevile, uhamishaji wa fedha kutoka nje ya nchi kupitia mfumo wa Malipo ya Taifa wa Papo kwa Papo umewezeshwa, ukiwa na gharama nafuu ya Shilingi 1,000, ambayo hulipwa na mtumaji. Pamoja na hayo, Benki Kuu iliweka ukomo wa gharama ada na tozo kuwa shilingi 3,000 kwa miamala ya shilingi 500,000 au zaidi ambayo hupitia mfumo wa GePG kutoka kwenye mifumo mbalimbali ya kidijitali. Aidha, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine wa mifumo ya malipo wanaendelea kufanya majadiliano kwa lengo la kung'amua maeneo yatakayosaidia kupunguza tozo na gharama na kubuni mikakati ya kuchagiza matumizi ya malipo ya kidijitali katika uchumi.

Mifumo ya malipo ya kikanda ikiwemo Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki (*East Africa Payment System – EAPS*) na Mfumo wa Malipo wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (*SADC-RTGS*), iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi katika kuchakata miamala baina ya nchi wanachama. Katika jitihada za kuongeza matumizi ya mifumo hii, Benki Kuu kwa kushirikiana na benki kuu za EAC na SADC ziliendelea kuchukua hatua mahsusi ili kukabiliana na changamoto zinazosababisha matumizi madogo ya mifumo hii.



Simu za mkononi zimeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kufikisha huduma za kifedha kwa wananchi ambao hawajafikiwa na huduma za kibenki. Kufuatia mwenendo huu, idadi na thamani ya miamala iliyofanyika kupitia simu za mkononi iliongezeka kwa asilimia 21.79 na asilimia 30.35, mtawalia, katika kipindi cha miezi tisa ya kwanza ya mwaka 2025/26 (Kielelezo 4.13a). Aidha ongezeko la matumizi ya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi limechangiwa na uwepo wa mifumo salama ya malipo, watumiaji kuongeza imani ya mifumo ya malipo na miundombinu wezeshi. Aidha, idadi na thamani ya miamala iliyofanyika baina ya makundi tofauti ya watoa huduma za fedha ambayo huchakatwa kupitia TIPS iliongezeka kwa asilimia 34.36 na asilimia 81.58, mtawalia (Kielelezo 4.13b).


Kielelezo 4.13a Malipo Kupitia Simu



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Kielelezo 4.13b: Miamala katika Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa Papo



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



SEHEMU YA TANO

5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI

5.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo mwaka 2026 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa nishati na kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa duniani. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuimarika kidogo mwaka 2027, kutokana na matarajio ya kutengemaa kwa masoko ya nishati na fedha duniani. Shirika la Fedha la Dunia (IMF) linakadiriya uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.1 mwaka 2026 na asilimia 3.2 mwaka 2027. Wakati huo huo, Benki ya Dunia inatarajia uchumi wa dunia kukua kwa kasi ndogo zaidi, kwa asilimia 2.6 na 2.7 kwa mwaka 2026 na 2027 mtawalia, huku OECD wakikadiriya ukuaji wa asilimia 2.9 na asilimia 3.1 mtawalia.

Kwa upande wa nchi zilizoendelea kiuchumi, IMF inatarajia uchumi wa Marekani na ukanda wa Ulaya kukua kwa asilimia 2.3 na asilimia 1.1, mtawalia mwaka 2026. Nchi zinazoibukia kiuchumi zinatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha kwa wastani wa asilimia 3. India inatarajiwa kuwa na kasi kubwa zaidi ya ukuaji wa uchumi, wa takriban asilimia 6.5, ukichangiwa na ongezeko la mahitaji ya ndani na mauzo nje ya nchi, kufuatia kupungua kwa ushuru kwa bidhaa zinazouzwa Marekani. Kwa upande wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kupungua kidogo hadi asilimia 4.3 mwaka 2026, kufuatia ongezeko la mfumuko wa bei, kupanda kwa bei za mbolea na gharama za usafirishaji zinazosababishwa na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi katika eneo la Mashariki ya Kati.



Mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kuongezeka mwaka 2026, ukibadili mwenendo wa kupungua ulioonekana mwaka uliotangulia, kutokana na kupanda kwa bei za nishati na bidhaa muhimu kwenye soko la dunia. Hususan, bei ya mafuta ya ghafi inatarajiwa kufikia dola za Marekani 82 kwa pipa mwaka 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani 67.74 mwaka 2025, kabla ya kushuka hadi dola za Marekani 75.97 mwaka 2027, kwa kadri mnyororo wa ugavi utakavyoimarika na masoko ya fedha kutengemaa. Kutokana na hali hii, IMF wanakadiria mfumuko wa bei kuongezeka kutoka asilimia 4.1 mwaka 2025 hadi asilimia 4.4 mwaka 2026, kabla ya kupungua hadi asilimia 3.7 mwaka 2027.

Katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5 mwishoni mwa mwaka 2026, kutoka asilimia 3.4 mwaka 2025. Ongezeko hili linaakisi athari za kupanda kwa bei za nishati katika soko la dunia, kushuka kwa thamani ya sarafu na kuongezeka kwa gharama za chakula. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.9 kufikia mwisho wa mwaka 2027, kadri misukosuko kutoka nje itakavyopungua pamoja na matokeo ya hatua zinazochukuliwa na nchi husika ili kuhakikisha utulivu wa bei. Ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei, nchi nyingi duniani zinatarijiwa kuongeza au kutobadili riba za sera ya fedha ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei.

5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani

Matarajio ya hali ya uchumi wa ndani ni ya kuridhisha kutokana na kutegemea sekta mbalimbali za uzalishaji, hivyo kusaidia kuhimili misukosuko kutoka nje ya nchi. Ukuaji halisi wa Pato la Taifa kwa Tanzania Bara unatarajiwa kuendelea kuwa imara, kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.6 mwaka 2027, ukichochea kwa kiasi kikubwa na ongezeko la uwekezaji wa serikali na sekta binafsi



na mauzo nje ya nchi. Shughuli zinazotarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa mwenendo huu wa ukuaji ni kilimo, madini, utalii na ujenzi. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.5 mwaka 2026 na asilimia 7.2 mwaka 2027, ukichagizwa na shughuli za ujenzi, utalii, na viwanda.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka, lakini ukibaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Kwa Tanzania Bara, mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa juu ya asilimia 4, wakati Zanzibar ukitarajiwa kubaki karibu na asilimia 5. Mwelekeo huu unazingatia matarajio ya uchumi wa dunia kukua kwa kasi ndogo zaidi ikilinganishwa na mwaka 2025, upatikanaji wa umeme wa uhakika pamoja na uwepo wa chakula cha kutosha. Aidha, matarajio haya yanazingatia kupanda kwa bei za mafuta na mbolea kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi Mashariki ya Kati. Hata hivyo, uwezekano wa mfumuko wa bei kuongezeka zaidi unategemea kwa kiasi kikubwa na muda na ukubwa wa mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati na athari zake kwa bei za nishati na bidhaa katika soko la dunia.



SEHEMU YA SITA

6.0 SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

Kwa kuzingatia mwelekeo wa uchumi sambamba na vihatarishi vilivyoainishwa katika Sehemu ya Tano, sera ya fedha kwa mwaka 2026/27 italenga kupunguza ukwasi ili kupunguza athari za kupanda kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia katika mfumuko wa bei wa ndani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) itaendelea kukutana kila baada ya robo mwaka kutathmini mwenendo wa uchumi na kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) ili kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Aidha, kwa kuangalia takwimu kuhusu mwenendo na matarajio ya hali ya uchumi nchini, umuhimu wa kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi utaendelea kuzingatiwa. Sambamba na hayo utekelezaji wa sera ya fedha utahakikisha kiwango cha kutosha cha ukwasi ili riba ya mikopo ya siku 7 kati ya benki katika soko la fedha inabaki ndani ya wigo wa CBR⁵.

Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuhimiza umuhimu wa matumizi ya malipo ya kidijitali na kuhamasisha wananchi na taasisi kutumia zaidi huduma rasmi za kifedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha upatikanaji wa takwimu kwa wakati na zenye ubora unaokubalika ili kusaidia kufanya maamuzi ya sera ya fedha. Sambamba na hilo, jitihada maalum zitaendelea kufanyika kuongeza uelewa kwa umma kuhusu mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu kama nyenzo kuu ya utekelezaji wa sera ya fedha. Jitihada hizi zitachagizwa na hatua zinazoendelea kufanywa na Benki Kuu ili kuongeza uwazi katika upangaji wa riba katika

⁵ Wigo wa Sera ya Fedha kwa sasa ni asilimia 1.5 juu au chini ya Riba ya Benki Kuu (CBR). (CBR \pm asilimia 1.5)



mazingira ya soko huria, na kuimarisha ufanisi wa sera ya fedha, huku maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) kuhusu Riba ya Benki Kuu yakitumika kama msingi wa upangaji wa viwango vya riba kwenye uchumi. Hii inajumuisha kuendelea kuelimisha wakopaji kuhusu Mfumo wa Kulinganisha Bei (*Price Comparator*) ili waweze kufanya maamuzi sahihi ya kifedha.

Aidha Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Katika soko la fedha, juhudi zitaendelea kufanyika ili kuboresha ufanisi, ikiwemo kuongeza uwazi na kupunguza vihatarishi. Benki Kuu itaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wengine ili kuboresha mfumo wa kisheria kwa lengo la kuwezesha utekelezaji kamili wa Mkataba wa Kimataifa wa Mauziano ya Dhamana za Serikali kwa Muda Maalumu (*Global Master Repurchase Agreement-GMRA*)⁶. Juhudi hizi zinatarajiwa kuwezesha mgawanyo sawa wa ukwasi ndani ya mfumo wa benki na kulinda uthabiti wa kifedha.

Kiwango cha ubadilishaji fedha za kigeni kitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko ili kuhakikisha sera ya fedha inaendelea kusadia kuhimili misukosuko ya kiuchumi ya ndani na nje ya nchi. Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni kwa kuzingatia Sera ya Ushiriki katika soko la fedha za kigeni, inayoruhusu ushiriki katika soko hili kwa lengo la kupunguza mabadiliko makubwa ya muda mfupi katika viwango vya ubadilishanaji wa fedha za kigeni, kuongeza akiba ya fedha za kigeni, kuchangia utekelezaji wa sera ya fedha, na kuongeza ukwasi katika soko la fedha za kigeni. Aidha, mfumo wa kielektroniki wa kuoanisha mahitaji na ugavi katika miamala (*Electronic Matching*

⁶ Mkataba wa makubaliano ya kisheria wa kimataifa unaosimamia miamala ya kubadilishana fedha dhidi ya dhamana (repo transactions) kwa kuweka mfumo wa usalama kwa wakopaji na wakopeshaji, pamoja na kudhibiti hatari inayoweza kutokea kutokana na sababu za kiutendaji au upande mmoja kushindwa kulipa pale muamala unapoiva.



System) utanza kutumika katika soko la jumla la fedha za kigeni. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi katika uendeshaji, uwazi, na upangaji wa bei, pamoja na kuimarisha nidhamu ya soko.

Benki Kuu pia itahakikisha akiba ya fedha za kigeni inaendelea kuwa ya kutosha kugharamia angalau miezi minne ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kama kinga dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi duniani. Hii itafanikishwa kupitia mikakati ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni, ikiwemo ununuzi wa dhahabu kupitia programu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani.



VIAMBATISHO



Jedwali 1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Tanzania Bara

Shughuli ya kiuchumi	Asilimia					
	2020	2021	2022 ^f	2023 ^f	2024 ^f	2025 ^a
Kilimo, Misitū na Uvuvi	5.2	3.7	4.3	4.3	5.1	5.5
Kilimo cha Mazao	5.3	4.0	3.5	4.3	4.5	5.0
Mifugo	5.1	4.8	4.9	4.9	5.1	5.3
Misitū	5.2	5.4	4.9	5.9	6.6	7.4
Uvuvi	5.9	-5.0	5.5	-1.2	6.0	6.3
Huduma katika Shughuli za Kilimo	6.5	3.2	3.0	6.9	4.6	6.4
Viwanda na Ujenzi	5.5	6.1	2.7	3.0	4.7	5.6
Uchimbaji Madini na Mawe	12.5	8.0	0.3	2.5	8.1	9.4
Viwanda	3.9	4.6	4.3	4.7	4.9	5.2
Umeme	-2.2	9.9	11.7	10.2	7.8	11.8
Maji safi na Maji taka	5.8	6.5	5.5	2.6	4.8	3.0
Ujenzi	3.8	6.0	2.5	2.2	3.0	4.0
Huduma	2.2	4.2	6.0	7.0	6.7	6.9
Biashara na Matengenezo	1.9	3.0	4.1	4.7	4.9	5.1
Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	5.4	5.2	6.5	7.0	7.2	8.0
Malazi na Huduma ya chakula	-14.8	4.6	11.5	7.3	4.1	3.6
Habari na Mawasiliano	9.1	9.3	5.4	10.7	11.2	8.8
Fedha na Bima	1.7	4.2	9.4	15.6	12.7	15.7
Upangishaji Majengo	1.3	3.1	4.3	3.9	4.0	4.2
Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	-5.0	7.1	4.3	4.4	4.2	5.6
Huduma zinazohusiana na Utawala	-4.9	1.6	6.5	6.9	2.1	4.3
Utawala na Ulinzi	10.4	2.6	2.3	1.9	7.0	5.8
Elimu	3.3	2.9	8.7	10.9	7.5	5.2
Afya na Huduma za Jamii	0.2	8.0	8.0	7.1	7.3	6.0
Sanaa na Burudani	-5.1	8.7	5.0	12.4	4.8	8.5
Huduma nyingine za Kijamii	4.6	7.1	6.8	8.7	5.3	5.4
Shughuli za Kaya katika kuajiri	3.1	3.1	3.7	4.3	2.9	2.8
Jumla ya Ongezeko la Thamani	4.0	4.6	4.5	5.1	5.7	6.2
Ongeza kodi katika bidhaa	-0.7	8.0	4.8	6.9	5.2	3.0
Pato la Taifa kwa bei za soko	3.6	4.9	4.6	5.2	5.6	5.9

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbithi: a Inamaanisha takwimu za awali

Jedwali 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Zanzibar

Shughuli za kiuchumi	Asilimia				
	2020	2021	2022	2023	2024
Kilimo, misitu na uvuvi	3.3	2.6	4.0	2.3	3.3
Mazao	1.3	2.2	6.1	2.8	6.4
Mifugo	8.2	3.0	2.3	-4.3	-10.8
Misitu na uwindaji	-4.4	4.0	2.9	6.4	0.1
Uvuvi	3.5	2.3	3.0	8.1	14.2
Vivanda	5.2	5.1	9.3	6.6	5.7
Uchimbaji madini na mawe	-6.0	9.9	9.1	10.4	17.0
Uzalishaji viwandani	6.5	1.1	8.1	6.9	3.3
Ume na gesi	-2.8	8.0	22.3	12.4	11.2
Maji	1.9	6.9	7.0	4.6	6.3
Ujenzi	6.5	8.9	10.2	5.5	6.3
Huduma	-1.0	6.9	7.7	9.9	9.0
Bashara na matengenezo	7.4	14.9	4.2	12.6	11.6
Usafirishaji na uhifadhi mizigo	-6.6	9.3	3.8	9.2	0.0
Malazi na huduma ya chakula	-12.7	6.6	11.7	8.2	13.7
Malazi	-11.3	6.5	12.3	7.8	13.2
Huduma za chakula na vinywaji baridi	-18.9	7.5	9.0	9.8	16.3
Habari na mawasiliano	-3.2	-16.3	2.5	-10.8	4.9
Fedha na bima	2.2	9.9	3.7	54.6	13.7
Upangishaji mejengo	6.8	7.0	7.1	7.2	7.3
Shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi	1.1	5.0	1.4	3.5	6.6
Huduma zinazohusiana na utawala	-4.6	6.6	-1.5	17.0	5.9
Usimamizi wa umma	13.2	5.3	8.2	2.1	4.0
Elimu	9.7	-0.3	9.8	3.7	7.0
Afya na huduma za jamii	1.4	2.4	8.9	15.8	8.2
Sanaa na burudani	-4.9	1.1	1.9	33.8	8.5
Huduma nyingine za kijamii	12.9	6.9	6.2	8.8	7.8
Huduma za ndani	3.2	3.2	2.9	2.6	3.2
Gharama za kifedha zilizojificha (FISIM)	11.7	2.8	6.5	38.1	37.1
Kodi za bidhaa	1.6	1.2	3.0	5.9	7.0
Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko	1.3	5.1	6.8	7.4	7.1

Chanzo: Ofisi ya Mtaalamu Mkuu wa Serikali-Zanzibar
Tanbihi: a inamaanisha takwimu za awali



Jedwali 3: Mfumuko wa Bei kwa Tanzania Bara

Makundi makuu	Uzani (%)	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jul-25	Agosto-25	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Dis-25	Jan-26	Feb-26	Mac-26	Apr-26
		Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia	Asilimia
Vyakula na Vinywaji Bandi	28.2	5.3	5.6	7.3	7.6	7.7	7.0	7.4	6.6	6.7	5.7	5.7	5.5	5.7
Vinywaji Vikali na Tumbaku	1.9	3.4	3.4	3.5	3.0	2.9	3.6	3.6	3.5	3.4	2.2	2.1	2.1	2.3
Mavazi na Viatu	10.8	2.0	2.0	2.0	1.9	1.7	1.9	2.0	2.0	2.0	1.2	1.1	1.3	1.6
Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	15.1	3.8	3.4	1.7	1.3	2.1	2.3	2.4	2.2	2.3	2.3	1.7	1.6	1.7
Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukurabati wa Makazi	7.9	2.3	2.3	2.0	2.4	2.4	2.8	3.1	3.0	3.0	2.7	2.5	2.3	2.6
Alya	2.5	1.5	1.7	1.8	1.6	1.3	1.2	1.2	1.3	1.3	1.1	0.9	1.1	1.6
Usafiri	14.1	2.1	1.7	1.6	1.2	1.4	2.1	1.7	2.9	4.1	4.2	4.0	4.2	9.2
Habari na Mawasiliano	5.4	0.1	0.1	0.0	0.2	0.4	0.2	0.3	0.3	0.5	0.9	1.1	1.0	1.0
Burudani, Michezo na Utamaduni	1.6	1.7	1.5	1.4	1.0	1.4	0.8	1.0	0.4	0.3	0.6	0.6	0.6	0.7
Huduma za Elimu	2.0	4.1	3.2	3.1	3.1	3.0	2.9	3.0	3.0	2.9	0.4	0.3	0.9	2.6
Migatawa na Huduma za Makazi	6.6	1.6	1.8	1.3	1.0	0.9	1.0	1.0	1.0	0.9	1.1	1.7	2.1	1.8
Huduma za Bima na Fedha	2.1	0.8	0.7	0.6	0.6	0.6	0.4	0.4	0.3	0.4	0.5	0.3	0.3	0.1
Usafi Binatsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma	2.1	3.0	2.0	2.0	2.0	2.3	2.3	1.6	1.7	1.2	3.2	3.2	3.3	3.5
Mchianganyiko	100.0	3.2	3.2	3.3	3.3	3.4	3.4	3.5	3.4	3.6	3.3	3.2	3.2	4.0
Mfumuko wa bei wa jumla														
Makundi mengine maalum														
Mfumuko wa bei wa msingi	73.9	2.2	2.1	1.9	1.9	2.0	2.2	2.1	2.3	2.5	2.2	2.1	2.1	2.2
Mfumuko wa bei usio wa msingi	26.1	5.7	5.6	7.1	7.1	7.3	6.7	7.3	6.2	6.7	6.0	5.9	5.6	6.3
Nishati, mafuta na ankara za maji	5.7	7.3	6.1	2.1	1.0	2.6	3.7	4.0	3.8	4.6	5.2	2.8	2.1	5.3
Huduma	37.2	1.1	1.0	0.9	0.8	0.8	1.3	1.0	1.6	2.0	4.6	2.2	2.4	4.0
Bidhaa	62.8	4.3	4.2	4.7	4.7	4.9	4.7	5.0	4.4	4.5	2.1	3.7	3.6	4.0
Huduma za elimu na bidhaa zineazhusiana na elimu	4.1	3.8	3.2	2.9	2.8	2.8	2.5	2.6	2.4	2.2	3.9	0.3	0.7	1.4
Mfumuko wa bei wa bidhaa zote isipokuwa vyakula na vinywaji bandi	71.8	2.3	2.1	1.7	1.5	1.6	1.9	1.9	2.1	2.3	2.2	2.1	2.1	2.1
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu														





Jedwali 4: Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar

	Asilimia												
	Apr-25	May-25	Jun-25	Jul-25	Aug-25	Sep-25	Oct-25	Nov-25	Dec-25	Jan-26	Feb-26	Mar-26	Apr-26
Mfumuko wa bei wa jumla	100.0	4.3	4.2	4.1	4.1	3.9	3.5	3.4	3.3	3.8	4.3	4.8	5.0
Mfumuko wa bei wa chakula	40.5	4.1	3.9	4.4	4.3	4.2	4.1	6.4	4.5	5.4	9.2	9.3	10.1
Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula	59.5	4.4	4.4	3.9	3.9	3.7	2.9	1.0	2.4	2.5	0.4	1.4	0.9
Minywaji vikali na tumbaku	0.2	-0.3	-0.2	-2.2	4.9	2.7	2.7	2.1	3.3	11.0	6.6	3.1	4.4
Mavazi na viatu	6.3	3.9	5.1	5.0	3.4	5.5	5.6	5.8	5.3	4.0	3.0	3.1	1.6
Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo	25.8	5.5	4.7	3.6	5.1	3.0	1.1	-3.3	0.0	0.6	-2.3	-0.2	-0.4
Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi	4.8	3.4	4.0	3.8	3.4	3.7	3.7	3.2	2.7	2.7	3.0	2.8	2.3
Alya	1.3	0.3	1.5	1.5	4.3	1.6	1.6	1.5	2.1	2.2	1.4	1.4	0.6
Usafiri	9.1	2.2	2.2	2.4	1.6	1.9	2.2	2.4	3.4	3.1	2.0	2.2	1.7
Habari na mawasiliano	4.2	2.0	2.2	2.8	2.3	2.7	2.7	2.3	0.7	0.1	-0.1	-0.2	0.0
Burudani, michezo na uamaduni	1.1	4.6	4.6	5.1	2.7	4.3	6.2	5.7	6.4	5.3	4.1	3.6	2.6
Huduma za elimu	1.6	2.6	3.8	2.1	4.3	3.8	3.8	3.1	0.8	1.1	1.9	1.9	1.6
Migahawa na huduma za malazi	1.4	0.6	0.6	0.6	3.8	1.6	1.6	1.9	1.9	2.2	7.1	7.1	6.8
Huduma za bima na fedha	0.5	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Usafi binatsi, hifadhi ya jamii na bidhaa na huduma mchanganyiko	1.7	3.5	4.9	4.8	5.0	5.4	5.8	5.4	4.5	4.8	1.8	2.2	2.0

Chanzo: Ofisi ya Mtafwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar

Jedwali 5: Takwimu za Kifedha

Shilingi Bilioni

	Apr-25	Mai-25	Jun-25	Jul-25	Augo-25	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Des-25	Jan-26	Feb-26	Marc-26	Apr-26
Rasilimali halisi za rife	14,658.6	14,028.1	15,509.5	15,726.1	15,766.0	15,986.7	15,715.4	16,298.6	15,286.5	15,950.0	15,749.5	15,245.6	14,553.0
Rasilimali halisi za ndani	38,679.1	39,313.4	39,973.8	40,565.0	41,669.9	41,957.4	44,073.3	44,560.0	45,702.6	46,155.7	47,319.8	49,001.1	50,538.9
Mikopo kwa sekta binafsi	38,755.8	39,792.0	40,549.0	40,972.2	41,530.9	41,998.9	42,386.9	43,385.5	44,603.1	45,171.4	46,054.2	47,216.5	47,919.3
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	53,337.7	53,341.5	55,483.3	56,291.1	57,455.9	57,854.0	59,788.6	60,858.6	60,989.1	62,105.7	63,069.3	64,246.7	65,091.9
Amana za fedha za kigeni (FCD)	13,846.3	13,543.4	13,768.3	13,653.2	13,696.3	13,337.2	13,882.1	14,056.5	13,255.7	14,103.2	14,589.7	14,998.4	14,989.0
Amana za fedha za kigeni (Dole milioni)	5,187.0	5,044.2	5,253.7	5,292.4	5,539.1	5,424.7	5,673.9	5,770.7	5,429.7	5,740.7	5,848.8	5,831.7	5,766.4
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	39,491.4	39,798.1	41,714.0	42,637.9	43,759.6	44,516.8	45,906.5	46,802.2	47,733.4	48,002.5	48,499.6	49,248.3	50,102.9
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	24,013.1	24,214.9	25,653.9	26,231.6	27,402.4	27,916.4	29,058.1	29,184.1	29,813.8	29,773.0	29,957.7	30,176.9	31,151.6
Fedha zilizo kwenye mzunguko	7,024.1	7,438.9	7,874.8	8,122.1	8,036.4	7,730.8	8,410.1	8,545.0	8,492.1	8,102.1	8,151.8	8,078.3	8,107.1
Amana za hundi	16,989.0	16,776.0	17,779.1	18,109.4	19,366.0	20,185.6	20,648.0	20,639.0	21,321.7	21,670.9	21,805.9	22,088.5	23,044.5
Viashiria vingine													
Fedha Taslimu	11,878.9	11,800.7	12,451.7	13,423.8	13,537.9	13,777.6	15,068.7	15,135.7	14,506.3	15,225.1	14,990.0	14,986.9	15,670.5
Akiba za banki	3,738.7	3,364.8	3,533.1	4,131.4	4,402.3	4,721.7	5,462.8	5,436.9	4,542.9	5,808.9	5,688.7	5,683.8	6,367.6
Fedha zilizo nje ya Benki Kuu ya Tanzania	8,140.2	8,435.8	8,918.7	9,292.3	9,135.6	8,995.9	9,605.9	9,698.8	8,865.4	9,416.2	9,301.3	9,315.1	9,302.9
Wastani wa Fedha Taslimu	11,779.6	11,803.9	12,165.4	13,157.5	13,523.6	13,838.6	14,530.7	15,282.6	15,302.9	14,923.0	15,067.6	15,227.2	15,447.2
Kiwango cha ubadilishaji fedha (mwisho wa kipindi) (Shilingi ya Tanzania/Dola Milioni)	2,669.4	2,685.0	2,620.9	2,579.8	2,472.7	2,458.6	2,446.7	2,435.8	2,441.3	2,456.7	2,491.1	2,571.9	2,599.4
Vivango vya ukaji wa kila mwaka (%)													
Fedha Taslimu	18.0	6.8	14.0	23.2	22.5	23.2	28.1	27.6	20.7	30.5	24.1	27.2	31.9
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	20.3	18.3	18.7	19.9	20.5	20.4	21.4	22.9	24.7	24.6	24.5	23.2	22.0
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	16.8	16.2	18.3	20.2	22.6	24.9	25.8	25.9	28.5	28.3	28.2	27.8	26.9
Mikopo kwa Sekta Binafsi	14.8	17.1	15.9	16.2	16.1	16.1	16.1	18.1	23.6	23.5	24.5	24.3	23.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Jedwali 6: Riba za Masoko ya Fedha na Mitaji

Aina ya riba	Asilimia												
	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jul-25	Agosto-25	Sep-25	Okt-25	Nov-25	Des-25	Jan-26	Feb-26	Mac-26	Apr-26
Riba katika soko la fedha baina ya mabanki													
Siku 1 (Overnight)	7.90	7.95	7.93	6.82	6.15	6.29	6.45	6.08	6.00	6.13	6.01	6.17	6.15
Siku 2-7	7.98	7.96	7.96	7.43	6.52	6.43	6.29	6.19	6.30	6.34	6.31	6.25	6.18
Riba ya jumla	8.00	7.98	7.94	7.35	6.48	6.45	6.38	6.30	6.29	6.40	6.34	6.32	6.26
Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabanki na Benki Kuu (Lombard rate)	8.00	8.00	8.00	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75	7.75
Riba ya mikataba ya mauziano ya dhamaana za muda mfupi (Reverse REPO rate)	7.21	7.21	7.21	5.77	5.78	5.76	5.76	5.77	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75
Riba ya dhamaana za serikali													
Siku 182	8.47	8.24	8.24	8.24	7.46	6.56	6.41	5.92	5.91	5.85	5.85	5.69	5.46
Siku 364	8.92	8.92	8.92	8.13	6.79	5.99	6.00	6.45	6.24	6.21	6.20	5.80	5.72
Riba ya jumla	8.86	8.89	8.89	8.13	6.83	6.03	6.27	6.25	5.87	5.89	5.68	5.21	5.06
Riba za hati fungani za serikali													
Miaka mwili	12.08	12.08	12.08	12.17	12.17	12.17	10.05	10.05	10.05	10.05	10.05	8.36	8.36
Miaka mitano	13.14	12.94	12.94	13.18	13.18	12.48	12.48	10.54	10.54	10.54	10.54	10.54	9.54
Miaka saba	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71	9.71
Miaka kumi	14.26	14.26	14.26	13.74	13.74	13.74	12.45	12.45	12.45	11.30	11.30	11.30	9.40
Miaka kumi na tano	14.63	14.63	14.63	14.63	13.91	13.91	13.91	12.08	12.08	12.08	10.78	10.78	10.78
Miaka ishirini	15.11	15.11	14.50	14.50	14.50	13.55	13.55	13.55	12.02	12.02	10.71	10.71	10.71
Miaka ishirini na tano	15.84	15.29	14.80	14.80	14.42	13.19	13.19	13.19	13.19	13.19	11.99	11.99	11.99
Riba ya Benki Kuu	6.00	6.00	6.00	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75	5.75

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania



Jedwali 7: Riba za Mabenki

Asilimia

Alina ya riba	Apr-25	Mei-25	Jun-25	Jul-25	Agg-25	Sep-25	Okf-25	Nov-25	Des-25	Jan-26	Feb-26	Mar-26	Apr-26
A: Shilingi ya Tanzania													
Riba za amana	2.89	2.52	2.90	2.90	2.90	2.92	2.93	2.88	3.02	2.94	2.98	2.89	2.91
Riba za jumla za amana za muda maalum	7.82	8.58	8.74	8.83	8.61	8.50	8.36	8.54	8.36	8.33	8.32	8.33	8.54
Miezi sita	9.36	9.82	10.28	10.28	10.44	10.12	10.06	10.01	9.96	10.20	10.26	10.51	10.35
Mwaka mmoja	9.27	9.72	9.79	9.88	9.99	9.84	9.21	10.02	9.58	9.70	9.82	9.60	9.81
Riba za amana za wateja wakubwa	10.52	10.64	11.21	10.72	10.99	11.05	11.22	11.67	11.66	11.74	11.48	11.57	11.37
Riba za mikopo za Jumla	15.16	15.18	15.23	15.16	15.07	15.18	15.19	15.27	15.24	15.10	15.11	15.11	15.33
Muda mfuupi (Hadi mwaka 1)	16.15	15.96	15.69	15.51	15.64	15.52	15.50	15.53	15.46	15.49	15.41	15.45	15.31
Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2)	16.33	16.35	16.49	16.41	16.45	16.26	16.42	16.42	16.42	16.73	16.70	16.53	17.19
Muda wa kati (Mwaka 2 hadi 3)	15.25	15.24	15.38	15.22	15.01	15.19	15.13	15.18	15.43	14.97	15.27	15.31	15.63
Muda mrefu (Mwaka 3 hadi 5)	13.88	14.19	14.35	14.39	14.02	14.26	14.24	14.43	14.29	14.05	13.96	13.95	14.56
Riba za mikopo za wateja wakubwa	12.88	12.99	12.68	12.56	12.72	12.84	12.40	12.61	12.38	12.25	12.19	12.21	12.56
B: Fedha za Kigeni													
Riba za amana	0.53	1.33	0.89	0.83	0.93	0.98	1.75	0.57	0.87	0.77	0.70	1.22	1.68
Amana za akiba													
Riba za jumla za amana za muda maalum	2.94	3.65	3.60	3.75	4.11	3.94	4.17	4.03	3.67	4.18	4.29	4.26	4.41
Miezi sita	3.55	4.61	4.92	4.94	4.60	5.10	5.05	5.25	4.82	4.66	4.80	4.97	5.03
Mwaka mmoja	3.01	4.10	4.06	4.00	4.47	4.61	3.86	3.47	3.19	3.82	4.43	4.35	4.83
Riba za mikopo za Jumla	8.89	8.81	8.70	8.82	8.59	8.43	8.71	8.52	8.61	8.57	8.61	8.70	8.96
Muda mfuupi (Hadi mwaka 1)	9.97	9.99	9.93	9.91	9.89	9.89	9.88	9.89	9.91	10.00	10.00	10.00	10.07
Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2)	8.16	8.39	8.22	8.23	8.11	7.49	7.73	7.65	7.68	7.68	7.72	7.69	8.82
Muda wa kati (Mwaka 2 hadi 3)	8.23	8.49	6.88	7.03	7.16	7.25	7.43	7.49	8.31	8.35	8.23	8.19	8.64
Muda mrefu (Mwaka 3 hadi 5)	8.36	8.17	9.43	9.42	9.30	9.16	9.23	9.30	8.50	8.64	8.83	9.09	9.19

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania





TAFSIRI YA DHANA MUHIMU

Riba ya Benki Kuu

Ni kiwango cha riba kinachoamuliwa na Kamati ya Sera ya Fedha na kutumiwa na Benki Kuu kusimamia, kuashiria mwelekeo wa sera ya fedha.

Mfumuko wa Bei wa Msingi

Ni kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma, zisizohusisha nishati, vyakula visivyochakatwa na huduma za umeme na maji kwa kipindi maalum. Bidhaa za vyakula visivyochakatwa, nishati, huduma za umeme na maji hazijumuishwi kwa kuwa bei zake hubadilikabadilika.

Uhimilivu wa Deni

Ni uwezo wa nchi kulipa madeni yake kwa wakati uliopo na baadaye bila kuhitaji msamaha wa deni au kuwa na malimbikizo ya madeni ambayo hayajalipwa (arrears). Kigezo muhimu cha kupima uhimilivu wa deni ni uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa (GDP).

Akiba ya Fedha za Kigeni

Akiba ya fedha za kigeni inajumuisha fedha na rasilimali zote za kifedha nje ya nchi ambazo zinasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Akiba hii hutumika kugharamia malipo ya nje, na pia kudhibiti kiwango cha nakisi ya urari wa malipo, kupitia ushiriki katika masoko ya fedha za kigeni. Akiba hii inajumuisha dhahabu-fedha inayomilikiwa na Benki Kuu ya Tanzania, haki maalum wanazopewa wanachama wa Shirika la Fedha duniani (IMF) kutumia kiwango cha fedha za kigeni (Special Drawing Rights (SDRs), akiba ya fedha za kigeni katika Shirika la Fedha Duniani (IMF), pamoja na rasilimali za fedha za kigeni zilizopo Benki Kuu ya



Tanzania kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kulipia bidhaa na huduma nje ya nchi.

Pato la Taifa (GDP)

Ni jumla ya thamani ya bidhaa na huduma zote zinazozalishwa katika uchumi ndani ya kipindi fulani. Bidhaa na huduma hizi huzalisha mapato halisi kwa uchumi ambayo hutumika ndani ya nchi au kwa ajili ya mauzo nje ya nchi. Pato la Taifa linaweza kupimwa kwa kutumia njia kuu tatu ambazo ni:

- Uzalishaji** – hupima thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa katika sekta zote za uchumi.
- Matumizi** – hujumuisha matumizi yote ya kaya, serikali, uwekezaji, na mauzo halisi ya nje.
- Mapato** – hupima mapato yaliyopatikana kutokana na uzalishaji, kama mishahara, faida, kodi na riba.

Mfumuko wa Bei

Kiwango ambacho wastani wa bei za bidhaa na huduma katika uchumi huongezeka kwa kipindi fulani. Kiwango hiki huwa kinawasilishwa kwa asilimia. Aidha, ongezeko la mfumuko wa bei huashiria kupungua kwa nguvu ya kununua au thamani ya fedha ya nchi husika.

Maoteo ya Mfumuko wa Bei

Ni makadirio ya matarajio ya kiwango cha mabadiliko ya fahirisi za bei kwa walaji (CPI) yanayofanywa na Benki Kuu, kulingana na tathmini ya hali ya uchumi wa ndani na mwenendo wa uchumi wa dunia. Makadirio haya hufanyika kwa kutumia uchambuzi kwa kutumia modeli za kiuchumi kwa kuzingatia utaalumu katika maswala ya kiuchumi. Kiashiria hiki huwasilishwa kama asilimia ya badiliko kwa mwaka.



Ujazi wa Fedha

Hujumuisha fedha zote zilizo kwenye mzunguko, nje ya mfumo wa kibenki na amana zote za wakazi wa hapa nchini zilizo kwenye mabenki. Kwa Tanzania ujazi wa fedha hutafsiriwa katika ngazi tatu ambazo ni ; Ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1), Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3).

- M1** — Hujumuisha fedha zilizo kwenye mzunguko, nje ya mfumo wa kibenki pamoja na amana za hundi za wakazi zilizo katika mabenki.
- M2** — Hii inajumuisha ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) pamoja na amana za akiba na za muda maalumu zilizo katika shilingi, zilizowekwa katika mabenki hapa nchini.
- M3** — Ujazi wa fedha unaojumuisha ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na amana za fedha za kigeni zilizowekwa na wakazi kwenye benki ndani ya nchi.

Kiwango cha Soko cha Ubadilishanaji wa Sarafu (NEER)

Ni kipimo kinachoonesha thamani ya sarafu ya nchi ikilinganishwa na wastani wa sarafu za nchi mbalimbali ambazo ni washirika wake wa biashara. Kwa ujumla, NEER hutumika kutathmini kama sarafu ya nchi inaimarika au inashuka dhidi ya sarafu za nje, hivyo kutoa viashiria vya awali kuhusu ushindani wa bidhaa za nchi katika soko la dunia.

Mfumuko wa Bei Usio wa Vyakula

Ni ongezeko la bei za bidhaa na huduma zote isipokuwa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kilevi.



Mkopo Chechefu

Ni mkopo ambao umeshindwa kurejeshwa kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba kwa kipindi kinachozidi siku tisini (90). Pia, mkopo unaweza kuelezwa kama chechefu endapo umeonekana kuwa wa kiwango duni (*substandard*), wenye mashaka (*doubtful*), au wa hasara (*loss*) kulingana na vigezo vilivyowekwa katika Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Usimamizi wa Mali Hatarishi), 2014, au kanuni nyingine zinazoongoza taasisi za fedha au taasisi za huduma ndogo za fedha. Mara tu mkopo unapobainishwa kuwa mkopo chechefu, huondolewa kwenye utaratibu wa kutoza au kutambua riba (nonaccrual basis).

Deni la Serikali

Hujumuisha madai yote ambayo Serikali Kuu inapaswa kulipa au madai yote yaliyodhaminiwa na Serikali. Kwa upande wa Tanzania, deni la Serikali limegawanyika katika makundi mawili ambayo ni; deni la ndani ambalo huchukuliwa mahushusi kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti, na deni la nje (ambalo huchukuliwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo). Deni hili hujumuisha madai yote ambayo Serikali inapaswa kulipa kwa wakopeshaji wa nje pamoja na madeni mengine ya nje ya Idara na taasisi za serikali yaliyochukuliwa chini ya udhamini wa Serikali.

Kiwango Halisi cha Ubadilishanaji wa Sarafu (REER)

Ni kipimo kinachoonyesha thamani ya sarafu ya nchi ikilinganishwa na wastani wa sarafu za nchi mbalimbali ambazo ni washirika wake wa biashara, baada ya kurekebishwa kwa kuondoa athari za mfumuko wa bei. Kipimo hiki cha huonesha ushindani halisi wa bei za bidhaa za nchi katika soko la dunia, kwa sababu huzingatia pia tofauti za mfumuko wa bei kati ya nchi.



Mikopo ya Muda Mfupi toka kwa Mabenki (repo)

Ni utaratibu ambao Benki Kuu hukopa fedha kutoka kwa benki kwa kuuza dhamana, kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo pamoja na kiwango fulani cha riba baada ya muda maalumu kwa kuzinunua tena dhamana hizo kutoka kwa benki zilizokopesha. Utaratibu huu hutumika kupunguza ukwasi katika uchumi.

Mikopo ya Muda Mfupi kwa Mabenki (reverse repo)

Ni utaratibu ambao Benki Kuu hukopesha fedha kwa benki kupitia ununuzi wa dhamana kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo pamoja na kiwango fulani cha riba baada ya muda fulani, kwa kuziuzua tena dhamana hizo kwa benki zilizokopeshwa. Utaratibu huu hutumika kuongeza ukwasi katika uchumi.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Barabara ya Jakaya Kikwete 40184,
Sanduku la Posta 2303, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 296 3182-7 au +255 26 22 223 2541
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: <https://www.bot.go.tz>